# MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO

**Toleo la 2**



## Hatua zaidi za kimsingi katika maisha ya Kikristo

Hili ni toleo la Pili katika Lugha ya Kiswahili la Maisha Mapya katika Kristo. Kwa mara ya kwanza kabisa kitabu hiki kilichapishwa kwa Lugha ya Kiispaniola na kilisomeka NUEVA VIDA EN CRISTO kilichapishwa na Iglesias Evangélicas Cenroamericanas na Camino Global huko Costa Rica. Makusudi yake ni kukupa wewe msingi imara katika maisha yako ya Kikristo.

Mara unapomalizo toleo la pili, endelea na toleo la Tatu mara moja

Kwa maelezo zaidi tuandikie barua pepe: **info@nuevavidaencristo.org**

Unaweza pia kupata nakala ya kitabu hiki na vitabu vingine kupitia mtandao huu: **www.NewLifeDiscipleship.com**

Matoleo yote yanapatikana pia katika Kiswahili, Kiengereza, Kifaransa, Kispaniola, Kireno. Matoleo mengine yanapatikana katika lugha zingine kama Kinyarwanda.

Umeruhusiwa kufanya nakala ya nyenzo hii kwa masharti kwambaunaelezea chanzo ya awali na kutofanya mabadiliko au nyongeza kwa maudhui yake.

© Mark Robinson
Haki ya kumiliki 2001,Tafsiri ya kwanza kwa Kiingereza 2004.

Kimetengenezwa na Mark Robinson
Camino Global Camino Global
8625 La Prada Dr., Dallas, TX 75228 USA

Februari 19, 2015

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| Mwongozo wa Mwalima ……………………………….……..... | | 4 |
| Hatua ya 1 | Kumjua Mungu ………………………........... | 6 |
| Hatua ya 2 | Kristo mfano wangu ………………….......... | 8 |
| Hatua ya 3 | Tumeitwa kutumikia ............................. | 10 |
| Hatua ya 4 | Mimi ni nani katika Kristo? ...................... | 12 |
| Hatua ya 5 | Vita vya kiroho ……………………….......... | 14 |
| Hatua ya 6 | Silaha ya Mungu ………………………........... | 16 |
| Hatua ya 7 | Samehe uwe huru ………………….......... | 18 |
| Hatua ya 8 | Nisamehe ……….……………….............. | 20 |
| Hatua ya 9 | Tumeitwa kuwa watakatifu …..…............ | 22 |
| Hatua ya 10 | Mkristo na Pesa yake ……………….......... | 24 |
| Hatua ya 11 | Ninaweza kufanya,lakini nifanye? ........... | 26 |
| Hatua ya 12 | Uchaguzi ……………………………......... | 28 |
| Hatua ya 13 | Kuwaeleza wengine habari za Kristo ……. | 30 |
| Hatua ya 14 | Wakati ujao……………….......................... | 32 |
| Hatua ya 15 | Mambo zaidi kuhusu wakati ujao ………. | 34 |
| Maelezo ya Ziada …………………………………....... | | 36 |

# MWONGOZO WA MWALIMU



1. Tunakupongeza kwa kukubali changamotola kuwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi kwa kutumia kitabu cha "Maisha Mapya Katika Kristo" kama mwongozo wako. Matokeo ya masomo haya yanaweza kuzaa tunda la milele.

2. Biblia iwe mamlaka yako katika kujibu maswali yote wakati wote. Mwanafunzi ni lazima atafute vifungu vya Biblia yeye mwenyewe, na kujaribu kujibu maswali kufuatana na jinsi Biblia inavyosema. Waumini wengine wapya wanahitaji kukabilishwa vyema jinsi ya kutafuta kifungu katika Biblia.

3. Kitabu hiki kinaweza kutumika kwa njia nyingi. Wakati mwingi, unaweza kusoma somo moja kwa Juma, huku ukiwatia moyo wanafunzi kufanya kazi zote katika kila somo.

4. Jaribu kufanya kipindi chako kisiwe cha muda mrefu sana.

5. Watie moyo wanafunzi kujibu maswali kwa kutumia maneno yao wenyewe, wakiepuka kunakili moja kwa moja kutoka kwenye Biblia. Hii itamsaidia mwanafunzi kuchanganua maana ya maandiko aliyojifunza.

6. Epuka kuhubiri. Tumia maswali ili uweze kugundua yale wanafunzi wanachoelewa na uweze kuwachochea kushiriki.

7. Jiandae vizuri wewe mwenyewe katika kila somo. Kama mwalimu, inakupasa kufahamu vifungu na mawazo makuu kwa kila kifungu. Unapojiandaa, ombea wanafunzi na moyo wako ili uwe tayari kwa somo.

8. Jaribu kufanya wanafunzi wafikiri juu ya matokeo ya masomo haya katika maisha yao. Wasaidie kuelewa matumizi kamili kwa vitendo. Maswali yaliyoko katika kisanduki pembeniyanakusudi la kufanya wanafunzi kuweka masomo hayo kwa vitendo katika maisha yao. Hivyo basi, yatumie.

9. Wasaidie wanafunzi waweze kuwa na tabia ya kuomba. Wafundishe kwa kuomba pamoja nao.

10. Ni muhimu kuelewa kwamba kufanya watu kuwa wanafunzi ni zaidi ya kujifunza masomo kumi na tatu katika kitabu cha 'MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO.' Uanafunzi una maana ya mabadiliko katika maisha ya mwanafunzi. Hiki kitabu ni msaada wa kutanguliza tu. Mwanafunzi anahitaji kuendelea kusaidiwa kutafuta namna ya kubadili tabia yake, namna ya kufikiri, mwenendo wake,na kadhalika.

11. Ni muhimu sana mwanafunzi kujifunza jinsi ya kuenenda kwa kusoma Biblia kila siku, kuomba, na kuweka vifungu vya Biblia kichwani. Unapoanza kila somo, chukua muda wa kumkumbusha mwanafunzi wako kifungu cha kukariri katika somo lililopita na kupate kuwauliza jinsi wanavyoendelea katika kusoma Biblia kila siku.

12. Uwe makini katika kutambua yale Mungu anayafanya katika maisha ya mwanafunzi. Katika kila somo, chukua muda wa kujibu swali lolote ambalo mwanafunzi wako anakumbana nalo, na kusaidia iwapo ana swala linalotatiza maisha yake. Yakupasa ufahamu kwamba unaweza kukosa muda wa kujibu maswali yote katika kila somo. Ikiwa hivyo, chagua maswali yaliyo muhimu sana, ambayo yanaweza kujadiliwa.

## Karibu katika jamaa ya Mungu

Ulianza maisha mapya ya ajabu pamoja na Kristo ulipomwamini. Lengo la kitabu hiki ni kukufanya uweze kujua Biblia isemavyo kuhusu maisha ya Mkristo. Kukua katika Kristo ni hatua kwa hatua. Kila siku tunapaswa kulishwa na kutembea pamoja na Kristo. Kadiri tutoavyo muda wetu kwa ajili ya ushirika wetu pamoja naye, ndivyo tutakavyopiga hatua hadi kukomaa.

## Muhtasari wa jinsi ya kutembea pamoja na Kristo

1. Soma Biblia kila siku ili kumjua Kristo vizuri.
2. Zungumza na Mungu kila siku kwa maombi.
3. Mruhusu Mungu atawale maisha yako, ukijisalimisha kwa mapenzi yake.
4. Zungumza na wengine kuhusu habari za Kristo.
5. Tafuta kuwa na ushirika na waumini wengine katika kanisa ambalo Kristo anahubiriwa.
6. Tafuta mwamini mmoja au wawili, ambao unaweza kuomba nao na kuwashirikisha mafanikio yako, na pia kushindwa kwako.
7. Onyesha kwa vitendo maisha yako mapya kwa kuonyesha upendo na shauku ya kuwajali wengine.

## Maisha inayotawaliwa na Kristo

Maisha ya Mkristo yanaweza kuwakilishwa na picha ya msalaba. Kristo ndiye kiini cha maisha yetu mapya. Tunaishi kwa kujisalimisha kwake.Mstari ulio wima, unawakilisha ushirika wetu pamoja na Mungu kwa maombi na kwa kusoma Biblia. Mstari wa mlalo unawakilisha ushirika wetu na watu wengine. Tunapaswa kutafuta ushirika na waumini wengine katika kanisa. Tunapashwa kuwaambia wale ambao hawajaamini habari za Kristo.






## Hatua ya 1
# Kumjua Mungu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Mungu, ni Mungu nafsi anayenijali mimi.
____ Naweza kupata kujua  kuhusu Mungu kwa majina aliyopewa.
____ Kuomba na kusoma Biblia  inatosha kumjua Mungu.

Ili kumfahamu mtu kiundani, ni lazima kuchukua muda wa kutosha kuwa naye kama inawezekana. Hii ndiyo njia ya kweli ya kuwafahamu watu au mtu. Ndivyo ilivyo hata katika mahusiano yetu na Mungu;unahitaji kuwa na wakati wa kutosha.

**MUNGU NAFSI**

Biblia inatufundisha kuwa Mungu ni  nafsi, si mtu aliyembali huko angani mahali Fulani, lakini yuko karibu, anavutiwa na maisha yetu, na anayejali kila jambo linalotokea.

1. Zaburi 139:1-3 Mungu anajua mambo gani kuhusu sisi? ____________

   ______________________________________________________________

2. Luka 5:18-20  Siku moja Yesu alipokuwa akiwafundisha makutano, watu waliwaleta rafiki zao waliopooza ili wapate kupona. Na wala hakuona usumbufu. Badala yake alipata muda na wakati wa kuhutubia juu ya mahitaji ya watu. Je, Yesu alifanya mambo gani mawili kwa watu walioopooza? Mstari 20,24 ______________________________

   ______________________________________________________________

3. Luka 5:30-32 Yesu alikosolewa alipomkaribisha  Mlawi mtoza ushuru ili afuatane naye. Kwa nini? Mstari wa 29-30 ____________________

   ______________________________________________________________

   Je, aliwajibu nini waliomkosoa? Mstari 31-32 ____________________

   ______________________________________________________________

4. Je, baada ya kusoma vifungu hivi vyote, unafikiri Mungu anavutiwa na maisha yako, hata kama umefanya makosa? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

   Kwa nini? _____________________________________________________

   ______________________________________________________________

5. Je, nawezaje kumjua Mungu kibinafsi?

   Yohana 5:39 ___________________________________________________

   Yeremia 33:3 __________________________________________________
   Mara zote Mungu yuko tayari kusikia furaha na huzuni zetu na hofu tuliyonayo na yuko tayari kutoa msaada kama tukimwita. Tunaweza kujisikia wapweke lakini kamwe si wapweke.

**NIFANYE NINI?**

Je, unapata wakati wa kupata kumjua Mungu binafsi?

❏ Ndiyo ❏ Hapana

Kama jibu lako ni hapana, je uko tayari kujitoa kwa ajili ya kujifunza Biblia na kuomba ili kumjua mungu vyema?



❏ Ndiyo ❏ Hapana

Hii ni ahadi ya maana sana. Leo ni siku ya kuanza! Kupata kumjua Yeye aliyekupenda na kuyatoa maisha yake kwa ajili yako.



**FIKIRI JUU YA HAYA:**

Juma hili, tafakari juu ya majina ya Mungu aliyopewa katika orodha hii.

Kama moja litakuwa na maana kwako basi liwekee alama, na umshukuru Mungu kwa ajili ya baraka ulizopokea kwa ajili ya kutafakari juu ya tabia ya Mungu.

- ❑ Mchungaji mwema (Yoh10:11)
- ❑ Tumaini langu (Zaburi 71:5)
- ❑ Mwamba wangu (Zab.18:2)
- ❑ Ngome yangu (Zaburi 18:2)
- ❑ Mwokozi wangu (Zaburi 18:2)
- ❑ Ngao yangu (Zaburi 18:2)
- ❑ Wokovu wangu (Zaburi 18:2)
- ❑ Ndiwe sitara yangu (Zab.32:7)
- ❑ Mwaminifu na WaKweli. (Uf.19:11)
- ❑ Hakimu wa kweli (2 Tim 2:5)
- ❑ Mpatanishi wangu (1 Tim 2:5)
- ❑ Amani yetu (Efeso 2:14)
- ❑ Mkate wa uzima (Yoh. 6:35)
- ❑ Mfalme wa amani (Isaya 9:6)
- ❑ Mkombozi wangu (Zab.19:14)
- ❑ Baba wa faraja (2 Kor.1:3)
- ❑ Kuhani mkuu (Waebrania 4:14)



**KUWA IMARA**

**Juma hili Soma Zaburi 1-7, (sura moja kwa siku).**

**Kariri Yohana 5:39**

***"Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake;na hayo ndiyo yanayonishuhudia."***

## KUMJUA MUNGU NI NANI

Mara zote Mungu anatafuta kuwa na mahusiano na sisi, siku za nyuma watu walimjua Mungu kwa majina yake, vyeo na tabia.

6 Ni jina gani lililotumika katika Mwanzo 17:1? ____________________

Inamaana gani katika maisha yetu kujua ya kuwa ni Mungu mwenye nguvu? ____________________

7 Mungu anaitwaje katika Kutoka 34:14? ____________________

Kwa nini anawivu? Mstari 14-15 ____________________
Kuabudu miungu ni kuweka kitu au mtu sehemu ambayo Mungu pekee ndiye anastahili katika maisha yetu. Inaweza kuwa labda kuweka mbele familia yako, michezo, kazi, marafiki, n.k.

Ebu weka alama kwa yale yanayochukua nafasi ya Mungu katika maisha yako. ❑ Marafiki ❑ Familia ❑ Kazi ❑ Michezo
❑ Runinga/picha za video ❑ Mtandao ❑ Muziki ❑ Pesa
❑ Mahusiano ya kimapenzi n.k. ____________________



8 Efeso 2:14 Inasema Mungu ni ____________________

Kwako, inamaana gani kusema Mungu ni amani yetu? ____________________

____________________

9 Katika Zaburi 23, Mungu anaitwa mchungaji wetu, ni nani kimsingi anahusika na kuchunga Kondoo. Soma, ukiangalia ahadi zinazopatikana katika kila mstari.

Mstari 1 ____________________

Mstari 2 ____________________

Mstari 3 ____________________

Mstari 4 ____________________

Mstari 5 ____________________

Mstari 6 ____________________

10 Unaposoma maandiko haya, kitu gani kinakuijia katika ufahamu na Moyo wako?____________________

- Mungu hutufariji. Je uko tayari kupokea kutufariji kwake au unapendelea kujisikitikia mwenyewe? ____________________
- Mchungaji hutuongoza katika njia ya haki. Je, njia zako zikoje? Je, ni za haki? ❑ Ndiyo ❑ Hapana
- Je, ni njia ipi unayoendelea nayo? Je, unaamani na njia uliyochagua? ____________________
- Je, unamaamini ya kuwa Mungu anajishughulisha na maisha yako? ❑ Ndiyo ❑ Hapana
- Je, unaamini kuwa unaweza kumjua Mungu kwa hakika kibinafsi? ❑ Ndiyo ❑ Hapana
- Je, uko tayari kuendelea kujisomea Biblia kila siku ili upate kumjua Mungu kwa hakika? ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Tafakari juu ya Mungu ni nani kwa kutumia msaada ulio katika mkono wako wa kushoto chini ya kichwa cha habari “FIKIRI JUU YA HAYA”.




## Hatua ya 2

# Kristo mfano wetu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Yesu mara zote anatupenda, hajali tunafanya nini.
____ Tumeitwa tufanyike kuwa sadaka ili tuwatumikie wengine.
____ Si uvumilivu na ni makosa kumwambia mtu maisha yako si sawa.

Kristo, ni mfano ambao kila mmjoa anaweza kumfuata. Alikuwa mkamilifu katika kila jambo, mtu pekee ambaye maisha yake na maneno yake yaliweza kusema: "Mimi ni njia" na "jifunzeni kutoka kwangu"

1. Ni nani aishiye ndani yetu? Wagalatia 2:20___________________________
   Kama Kristo anaishi ndani yetu, sasa tunapaswa kuishi kwa namna gani?
   ______________________________________________________________

   Fuata mfano wake katika maeneo yafuatayo:-

**UPENDO**

2. Ni kwa jinsi gani Yesu alionyesha upendo? Warumi 5:8 ________________
   Upendo wa Kristo katika vifungu hivi ni:-
   - ❏ Hauna masharti (anatupenda bila, kujali sisi ni akina nani au tukoje)
   - ❏ Wenye masharti (anatupenda wakati tunapokuwa wazuri).

3. Yohana 15:13 "Hakuna aliye na upendo mkuu kuliko huu, wa mtu __________________________ kwa ajili ya rafiki zake.

4. Leo, Je tumeitwa kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa pia? ❏ Ndiyo ❏ Hapana
   Kupenda kama Kristo inamaana ya kuwa tayari hata kujitoa sadaka kama Kristo alivyofanya kwa ajili yaw engine. Hii haina maana ya kuwa ni kufa kwa ajili yao, lakini ni kuwapa Muda wetu, kuwasikiliza, kuwasaidia, kuwatia moyo katika kuhangaika kwao,n.k.

5. Wengine watajuaje ya kuwa sisi ni wanafunzi wa Kweli wa Yesu Kristo? Yohana 13:34-35 ________________________________________________

6. Utawezaje kubaki katika upendo wake? Yohana 15:10 ________________
   ______________________________________________________________

**UNYENYEKEVU NA HUDUMA**

7. Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa Kristo? Mathayo 11:29 ___________
   ______________________________________________________________

8. Soma Wafilipi 2:5-8. Kristo, ambaye ni Mungu aliishi Mbinguni na aliishi mbali na dhambi hapa Duniani. Badala yake, mstari wa 7 unasema akajihesabu si kitu, akachukua namna ya_____________. Ina maana gani kuwa mtumishi? ________________________________________________

9. Unyenyekevu wa kipekee kabisa ambao Yesu aliuonyesha ni kifo chake pale msalabani (mstari 8), kusulubiwa hakukuwa tu na maumivu makali, lakini pia kwa aibu kubwa. Alikufa katikati ya wezi, akiwa uchi, akateswa msalabani kama mharifu badala ya mfalme. Mstari wa sita unatuambia

**JAMBO LA KUTAFAKARI**

Kristo alifuata mapenzi ya Baba yake. Kwa kuwa mimi ni wake nitafanya nini ili kumtukuza katika maisha yangu?

________________________
________________________
________________________
________________________
________________________

**KWA AJILI YA MFANO WA KUIGA.**

Kristo alimwomba baba yake hata kabla hakuja pambazuka. Wewe hufanya nini unapoam-ka?



Kama hauombi hiyo inamaana gani kulingana na mtizamo weyu wa kimungu?

________________________
________________________
________________________
________________________
________________________

**MAMBO YA KUFANYIA KAZI**

Weka alama katika orodha ifuatayo mambo ambayo uko tayari kuyafanyia kazi.

- ❏ Nitaomba kila siku, niki-omba kuwa kama Yesu.
- ❏ Nitayatafuta mapenzi ya Mungu kwa kupitia maandiko na maombi.
- ❏ Kila siku nitajikabidhi kwake, nikimpa nafasi ya kutawala kila sehemu ya maisha yangu.

kuiga unyenyekevu wake. Kwa namna gani? Mstari wa 3-4 ____________

________________________________________________________________

10. Kulingana na Luka 6:31, ni njia ipi nzuri ya kuwatumikia wengine?

________________________________________________________________

## HURUMA

11. Kulingana na Mathayo 9:35-36, Yesu aliwaonea ____________________ makutano. Kwa nini? ____________________________________________

12. Je, unawatizamaje wasio amini wanaoisha karibu nawe? Je, ni rahisi kuwakosoa kuliko kuwaonea huruma ______________________________

13 Mafarisayo wakiwa wanatafuta kumtega Yesu, walimleta mwanamke aliyefumaniwa akizini. Wakimnukuu Musa, wakamuuliza Yesu kama mwanamke huyo anastahili kupigwa mawe hadi afe, na Yesu akawajibu, Yeyote kati yenu asiye na _____________ na awe wa kwanza __________ __________________________________________________” Yohana 8:7

14. Je, ni kwa jinsi gani mtizamo wa Yesu juu ya huyu mwanamke unatofautiana na mtizamo wetu wa leo tunapomwona mtu akijihusisha na dhambi? Yohana 8:10-11 ______________________________________________

________________________________________________________________

15. ❑ KWELI ❑ SI KWELI: Kuonyesha huruma kwa watenda dhambi ni kama kawafanya waendelee au ni kama kufumbia macho tabia zisizofaa.

Ingawaje Yesu alimwonea huruma, Yesu pia alimwambia “nenda ______________________________________.” Mstari wa 11.

Huruma ya kweli ni tofauti na “ustahimilifu” maana hutupelekea kuwapenda wanaotenda dhambi, na wala si kuvumilia tabia zao.

## UJASIRI WA KUKEMEA MAKOSA

16. Ni kwa jinsi gani Yesu aliukemea unafiki wa Mafarisayo? Mathayo 23:27

________________________________________________________________

17. Kukemea unafiki na dhuluma kunahitaji ujasiri. Je ni sahihi kijificha kwa kusema, “ sitaki kumkwaza mtu yeyote?” ___________________________

## MAOMBI

18. Ni mfano gani Yesu alitupa katika Marko 1:35? ______________________

Kwa nini unafikiri ni muhimu kusali/kuomba asubuhi na mapema?

________________________________________________________________

19. Siku moja Yesu aliomba usiku kucha kabla ya kufanya maamuzi ya muhimu sana. Ni kitu gani cha muhimu sana alichokuwa akiomba juu yake? Luka 6:12-13 ____________________________________________

Mungu anatarajia kwa kila muumini kutafuta mapenzi ya Mungu katika maamuzi yote wanayofanya. Zaidi ya hayo, pia ni muhimu kujua kuwa Yesu hakuwa akiomba wakati anapotaka kufanya maamuzi pekee, lakini pia kutafuta ushirika mtakatifu na Baba yake.



**TAFAKARI JUU YA HAYA:-**

Je, kuna mienendo ambayo inaweza kutuzuia kufuata mfano wa Kristo kama tulivyoona katika somo hili?

Weka alama katika mambo yafuatayo ambayo yanaweza kukuzuia wewe kuishi maisha ya unyenyekevu na huduma.

- ❑ Kuwa na wasiwasi na kila kitu
- ❑ Mgumu wa kusamehe wengine
- ❑ Majivuno
- ❑ Kutokuwa mvumilivu kwa wengine
- ❑ Kutowapenda wengine.
- ❑ Wivu
- ❑ Tamaa
- ❑ Ubinafsi
- ❑ Hasira
- ❑ Mawazo maovu
- ❑ Kuwa na mawazo tofauti juu ya mahitaji yaw engine.
- ❑ Na mengineyo

______________________

______________________

______________________



**KUWA IMARA**

**Soma Efeso 1-6 na Zaburi 8, (sura moja kwa siku kwa juma lote hili).**

***Kariri Mathew 11:29***

***"Jitieni Nira yangu, na mjifunze kutoka kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo;nanyi mtapata raha nafsini mwenu;"***



### Hatua ya 3
# Tumeitwa kuhudumu

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Njia pekee ya kumtumikia Mungu ni kwa kupata wadhifa kanisani.
____ Wakristo wenye nguvu pekee ni wale walio na uwezo wa kuhubiri.
____ Kila aliyeamini anao uwezo wa kuhudumu.

**KUFUATA MFANO WA YESU**

Huduma nis sehemu ya maisha ya Mkristo, lakini si kila mtu anafahamu vyema maana ya kutumika. Acha tuone ni mambo gani Yesu aliwafundisha wanafunzi wake juu ya umuhimu wa huduma.

1. Soma Mathayo 20:26-27 na ujaze nafasi zilizoachwa wazi. Bali mtu yeyote anayetaka kuwa ____________ kwenu na awe ___________ wenu; na mtu yeyote anayetaka kuwa wa ____________ kwenu na awe _________wenu.

   Wale wanaojitazama wao wenyewe na maslahi yao binafsi kamwe hawataipata furaha waitafutayo.

2. Unafikiri ina maana gani kuwa “mtumishi” wa wengine? ______________

   ________________________________________________________________

   Kuhudumu ina maana ya kujitoa dhabihu, lakini kujitoa dhabihu kumeambatana na kuridhika au kwa lugha nyingine kukubaliana na hali fulani. Zaidi ya kuwa na mzigo, huduma ya kujitoa kama dhabihu kwa wengine ni heshima ya kipekee.

3. Mfano mahiri wa kufuata ni ule uliotolewa na Yesu katika Mathayo 20:28 Kama vile mwana wa Adamu asivyokuja _____________ bali ____________ na kutoa _____________________________ iwe fidia kwa wengi.

4. Toa mfano wa namna ambavyo unaweza kuyatoa “Maisha yako” kwa ajili ya kuwatumikia wengine:___________________________________________

**KUTUMIA KARAMA ZAKO**



Biblia inatuambia kuwa Mungu amempa karama kila aliye mshiriki katika kanisa lake. “Karama ya kiroho” kipawa au uwezo Fulani unaochangia katika kuliimarisha na kulikuza kanisa.

5. Ni waumini wapi waliopokea karama za kiroho? 1 Wakor 12:7 __________ Kumbuka:ufunuo wa Roho mtakatifu mahali hapa ni kwa ajili ya karama za kiroho.

6. Karama zako ni kwa ajili ya matumizi yapi? 1 Petro 4:10 _______________

   ________________________________________________________________

   Karama zatoka kwa Mungu na kamwe si kwa ajili ya faida binafsi, lakini pia kwa ajili ya faida ya waumini wengine katika kanisa.

Soma Warumi 12:3-5 na ujibu maswali yafuatayo:

7. Nijitizameje? Mstari 3 _____________________________________________

   ________________________________________________________________

**JAMBO LA KUTAFAKARI**



Tengeneza orodha karama za kiroho ambazo unazo na eleza jinsi ambavyo unaweza kuzitumia katika kanisa lako na katika jamii yako

________________________
________________________
________________________
________________________
________________________

ukimwonyesha orodha, muulize jinsi unavyoweza kuzitumia karama hizi.

**FIKIRI JUU YA HILI.**

Kanisa linafananishwa na mwili wa mwanadamu. Je, umewahi kukiponda kidole gumba chako na bado ukaendelea kukitumia? Si rahisi si ndiyo? Sasa ebu fikiri ni jinsi gani kanisa linalemazwa wakati washirika wanaposhindwa kuzitimia karama zao.

Je, ni kwa jisni gani waumini wengine wanaathirika unaposhindwa kuutumia uwezo na kipawa ulichopewa?

________________________
________________________
________________________
________________________
________________________



**KWA KUJIFUNZA ZAIDI**

Mtumishi wa Kristo anapaswa aweje?

Soma vifungu vifuatavyo huku ukinukuu mwenendo au tabia za mtumishi zilizotajwa katika kila kifungu. 1 Wakor 15:14

______________________

______________________

______________________

Wafilipi 2:3-4

______________________

______________________

______________________

1 Wakor 10:31

______________________

______________________

______________________

Wakolosai 3:23-24

______________________

______________________

______________________



**KUWA IMARA**

**soma wakolosai 1-4**
**na Zaburi 9-11**
**(Sura moja kwa siku kwa muda wa wiki moja)**

***Kariri Mathayo 20:27-28***

***"…….na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu;kama vile mwana waAdamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."***

8. Kanisa linaitwa mwili wa Kristo na linafananishwa na mwili wa mwanadamu. Mstari wa 5 sisi ni ______________katika_________________

   Na matokeo yake inampasa kila aliyeamini kuutafuta umoja katika mwili kwa kuwatumikia wengine.

9. Mstari wa 4 unasema kuna ________________ katika mwili, lakini havitendi ___________________. Kwa kuwa hali hii ndivyo ilivyo je, inatupasa kuwa na wasiwasi kwa kutokuwa na karama zote kwa wakati mmoja?

10. Watu wapi ni wa Muhimu sana kanisani kwako? ❑ Mchungaji
    ❑ Waalimu ❑ Wanamuziki ❑ kila mmoja ni muhimu

11. Kulingana na 1 Wakorintho 12:20-22, je, kuna washiriki katika kanisa ambao ni wa muhimu sana kuliko wengine? ______________________ kwa nini?__________________________________________________________

    Kulingana na karama za kiroho hakuna nafasi ya majivuno wala dhuluma. Wale wanaowadhulumu wengine kwa karama zao hao bado hawajavielewa vizuri vifungu hivi vinafundisha nini. Mungu anakazi tofauti tofauti kwa waumini tofauti tofauti. Karama za watu wengine ni za kuona kwa macho kwa mfano wale wanaohubiri na kufundisha mibarani, lakini kuna wengi ambao karama zao ni za muhumu sawa na hao wanaohubiri na kufundisha, lakini zinatumika lakini hazionekani sana kwa macho.

12. Aya ifuatayo ina orodha ya karama tofauti tofauti kama vile kusaidia, kufundisha, kutoa, ushauri, utawala, Huruma, uinjilisti, uchungaji n.k. Efeso 4:11, Warumi 12:6-8, 1 Wakor 12:7-10, 28-30

13. Kama tulivyoona si kila muumini anakarama sawa na mwingine. Kwa nini ni muhimu kulifahamu hili? ____________________________________________

    ____________________________________________________________

    Usijitenge kamwe kutoka katika mwili huo. Kanisa linaweza kusonga mbele pale tu sisi sote tutakapotumia karama zetu kwa pamoja ili kulifanya kanisa liwe kamili na lenye afya.

14. Kundi linaathirika kiasi gani iwapo washiriki watashindwa kuzitumia karama zao? ________________________________________________________

## NITAZITAMBUAJE KARAMA ZANGU?

Njia bora zaidi ya kutambua karama zako ni kwa kusaidia mahali kunapokuwa na uhitaji. Baada ya kujihusisha katika huduma mbalimbali utaweza kugundua kuwa ni kazi ipi Unaimudu zaidi, na ipi hauiwezi. Usikie ushauri wa waumini waliokomaa wanaoona uwezo na udhaifu wako.

15. Ni karama zipi unafikiri unazo? ____________________________________

    ____________________________________________________________

## MUHTASARI



- Biblia inatufundisha kuwa kilamuumini yampasa kutumika na wala si kutumikiwa.
- Mungu ametupa karama ambazo zitachangia katika kukua kwa kanisa, na muhimu sana kutambua nafasi yetu katika Kristo.

## Hatua ya 4

# Mimi ni nani katika Kristo?



Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)

____ Sasa mimi ni muumini, na ni mshirika katika familia mpya.

____ Tuna nafasi ya kipekee kabisa katika Kristo.

____ Nina msaada wa kibiblia ili kuendelea kutunza heshima yangu kwa kiwango cha juu.

Kwa kuwa adui yetu, Shetani ni mwerevu na atajaribu kutuchimbia shimo ili tutumbukie, kwa kutufanya tujione kuwa sisi ni wakosaji hali itakayotupelekea kushindwa kiroho. Je, sisi ni wa muhimu kweli kwa Kristo au tunajidanganya?

**MIMI NI MWANA WA MUNGU**

1. Elezea kifungu hiki kinamaana gani kinaposema, "wote waliompokea" katika Yohana 1:12 ________________________________

2. Huwa kinatokea nini mtu anapompokea Kristo? ____________________ ______________________________________. Watoto wananafasi ya muhimu sana katika familia, hasa familia husika kama ni ya Mungu.

**MIMI NI HEKALU LA MUNGU**

3. 1 Wakorintho 6:19 inasema kuwa kila muumini ni Hekalu au mahali pa Mungu kukaa. Kulingana na kifungu hiki ni nani aliye ndani ya kila muumini? ________________________________

4. Katika kifungu hiki, usemi huu una maana gani, "ninyi si mali yenu wenyewe?" ________________________________

5. Kama Mungu Roho mtakatifu huishi ndani yetu, je Shetani anaweza kutufanya lolote analotaka kwetu? 1 Yohana 4:4 ❏ Ndiyo ❏ Hapana kwa nini?

**MIMI NI MTAKATIFU, NIMEITWA KUWA MTAKATIFU**

6. Watakatifu walikuwa ni akina nani, ambao Paulo anawaongelea katika Wafilipi 4:21?________________________________

7. katika 1 Wakorintho 1:2 alikuwa akiwaandikia wale _______________ katika Kristo Yesu, na walioitwa ________________. " Waliotakaswa" kuna maanisha ukweli kwamba kila muumini amefanywa kuwa mtakatifu, si kwa juhudi zake mwenyewe, lakini ni kwa kazi ya Kristo. Kutakaswa maana yake ni kutengwa na mambo ya Dunia yanayoonekana ya maana, ili kuishi kwa ajili ya Mungu.

**MIMI NI KIUNGO KATIKA MWILI WA KRISTO**

8. Katika 1 Wakor 12:17, " wewe ni ____________________ na kila mmoja wenu ni sehemu ya huo mwili", mtu anapompokea Kristo, anabatizwa na Roho mtakatifu, ambayo ni kusema, kufanyika kuwa sehemu ya mwili wake Kristo(1 Wakor 12:13) "Mwili wa Kristo" ni sawa na kanisa la ulimwengu, likijumuisha waumini wote Dunia nzima. (Efeso 1:22-23)

**JAMBO LA KUFANYA**

Kila siku juma hili, soma kifungu kimoja au zaidi kati ya hivi vilivyoorodheshwa na uangalie nafasi yako katika kanisa.

- 2 Wakor 5:17
- Warumi 6:1-11
- Warumi 6:12-23
- Yohana 15:1-5
- Yohana 15:15
- Wagalatia 4:6-7
- Efeso 2:4-7
- Wafilipi 3:20
- 1 Petro 2:11

Baada ya kuvitafakari vifungu hivi unafikiri nafasi yako ni ipi katika kanisa?




**FIKIRI JUU YA HILI**

Kuelewa nafasi yetu katika kristo kitatusaidia angalau maeneo matatu katika maisha yetu.

1. Kutatusaidia kudumisha heshima tukizingatia vile tulivyo na vile Mungu anavyofikiri juu yetu.

2. Kadri tunavyoishi katika haki kila siku, tutapata kuufahumu kwa undani zaidi mpango wa Mungu juu ya maisha yetu.

3. Tutakuwa imara katika vita vyetu na Shetani, ulimwengu na mwili.

**NAANGALIA SURA YA NYUMA**




Familia yako ilikuwaje ulipokuwa mtoto?

Je, ulipata haya yafuatayo?

Upendo ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Usaidizi ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Watu kukuelewa ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Kutiwa moyo ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Ulinzi ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Kama hukupata upendo na ulinzi kama mtoto, yote hayo yamekwisha pita. Leo unayo familia mpya katika Kristo. Mwombe Mungu ili akuondolee machungu na umshukuru kwa ajili ya wale aliokupa katika familia hii mpya.



**KUWA IMARA**

**Juma hili Soma Mathayo 1-7 (sura moja kwa siku)**

***Kariri Wakolosai 3:1***

***"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu."***

9. Kulingana na Waefeso 2:19 sisi si wageni tena ………..bali wenyeji pamoja na watakatifu, nasi ni wa ______________________ya Mungu.

10. Kama sisi ni wa nyumba ya Mungu, na waumini wengine ni ____________ ________________________________

11. Tafakari jinsi familia inavyofanya kazi. Je, inamaana gani kwako kujua ya kuwa uko katika familia mpya? ____________________________________ ____________________________________________________________

    Kama tulizaliwa katika familia ambayo ilikuwa haifanyi kazi sawasawa, ambapo hapakuwa na upendo wala kukubalika, sasa jua ya kuwa unayo familia mpya ambayo itakusaidia na kukutia moyo.

**NIMEKUFA KWA DHAMBI**

12. Wagalatia 2:20 inasema tume_____________________________, je ina maana gani "Kusulubiwa pamoja na Kristo"? Angalia sehemu nyingine ya kifungu ili uweze kujibu. ________________________________________ ____________________________________________________________

13. Wakolosai 3:1, Zaidi ya kusulubiwa pamoja na Kristo, pia tuli ___________ ___________________pamoja na Kristo. Je, yatupasa kuishi vipi? Mstari 1 ____________________________________________________________

14. Katika kifungu hicho hicho, sentensi inayosema "yafikirini yaliyo juu" una maanisha nini?_____________________________________________________

**SINA HUKUMU TENA**

15. Warumi 8:1, Hakuna _______________ kwa wale walio katika Kristo Yesu.

16. Warumi 5:1, Basi tukiisha _________________itokayo katika Imani, na tuna ________________ kwa Mungu. "kuhesabiwa haki"kuna maana ya kwamba

    Mungu ametangaza haki kwa sababu ya kifo cha Yesu kwa niaba yetu. Waumini wengi huwa inakuwa ngumu kuamini kuwa kweli Mungu amewasamehe, wakiamini kuwa dhambi zao ni nyingi sana wala si rahisi kusamehewa. Na matokeo yake wanaendelea kujisikia wenye hatia na hatimaye wanashindwa kuuona ushindi katika Kristo Yesu. Ndiyo maana vifungu hivi viwili ni muhimu sana;vinatuweka huru.

**MIMI NI WA KIPEKEE**

17. Kulingana na 1 Petro 2:9 sisi ni nani sasa katika Kristo?

    a. ______________________________ b. ______________________________

    c. ______________________________ d. ______________________________

18. Ina maana gani kwako, kujua ya kuwa unanafasi maalumu kati Kristo? ____________________________________________________________

19. Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi, je, maisha yangu inanipasa niishi-je? 2 Wakor 5:15 ______________________________________________




## Hatua ya 5
# Vita vya kiroho

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Shetani huwashambulia waumini kwa kuwaonyesha dhambi zao zote.
____ Shetani hutumia uongo ili kuyakusa mambo ili kutuogopesha.
____ Wakristo wote wanalindwa wasishambuliwe na Shetanni.

### VITA VISIVYOONEKANA KWA MACHO

1. Waefeso 6:12, inazungumzia vita hivi, kulingana na kifungu hiki kushindana kwetu si juu ya ______________________________ , bali ni juu ya ______________________________________________

2. Unafikiri hawa "Watawala" na "Mamlaka" ni wapi hasa? ____________ ______________________________________________

3. Shetani anajaribu kutufanya nini? 1 Petro 5:8? ______________________ Muumini anapaswa kufanya nini? Kifungu cha 9 ____________________

**Adui yetu ni nani?**

Watu wengine hufikiri shetani ni mchekeshaji maarufu sana,akiwa amevalia mavazi mekundu, mapembe kichwani na mkia mrefu sana. Inawezekana shetani mwenyewe ndiye mwamdishi wa wazo hilo, kwa sababu Biblia inamwelezea tofauti kabisa. Shetani pamoja na washirika wake, mapepo, ni malaika walianguka. Shetani alikuwa mmoja wa Makerubi,akiwa mzuri na mkamilifu, hadi alimuasi Mungu (Ezekieli 28: 14-15). Tangu siku hiyo ametangazwa kuwa adui wa Mungu na watu wake.

### MBINU ZA ADUI

Shetani hutumia mbinu nyingi, akizingatia mtu anayemshughulikia au hali iliyopo. Wakati mwingine anafanya kazi wazi wazi kupitia dini za uongo, uganga wa kienyeji na uchawi. Yeye mara nyingi ni mwerevu sana, hivyo wakati mwingine ni vigumu kugundua ushawishi wake katika jambo fulani. Kwa kadri tunavyopata kuzielewa mbinu zake ndivyo, tutakavyoweza kumpinga.

4. Soma kumbukumbu ta Torati 18:10-12. Inasema nini kuhusu mtu apigaye bao, apandishaye pepo, alogaye, awaombaye wafu,nk…? ____________ ______________________________________________

   Kupiga Ramuli ni kubashiri mambo ya mbeleni yatakayotokea ni elimu iliyojificha katika uchawi. Waganga wa kienyeji hutumia vitu kama kupiga ramuli, n.k. na wakati huo huo hudai kuwa wanauwezo wa kujua mawazo ya mtu bila yeye kuwaambia.

5. Kulingana na 2 Wathesalonike 2:9, baadhi ya watumishi wa shetani watatenda kwa ______________________, _____________________ na ____________________ Shetani hutumia nguvu zake kuwadanganya watu, kuwaogopesha na wakiamini kuwa haonekani, nay a kuwa atawapa uwezo, nguvu na upendeleo maalumu.

6. Yohana 8:44b inatuambia "Yeye ni ____________ na ni baba wa ________ ______________________________________________

**UCHAMBUZI WA NDANI ZAIDI**

Shetani hutumia uongo ili kuwatisha na kuwadanganya watu wa Mungu, akijaribu kuwapotesha katika njia iliyo ya kweli.

Orohesha baadhi ya uongo ambao amejaribu kuutumia katika maisha yako.

________________________
________________________
________________________
________________________
________________________
________________________
________________________
________________________
________________________
________________________



**KUWA IMARA**

**Juma hili Soma Mathayo 8-14 (sura moja kwa siku).**

***Kariri Yakobo 4:7***

***"Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia."***

**JAMBO LA KUTAFAKRI**

Mara kwa mara kwa sababu ya kutokuelewa kwetu tunajikuta tumeingia katika hali ya hatari…
Kama umewahi kujihusisha na jambo lolote lililo katazwa, katika visanduku vifuatavyo weka alama ya mambo/jambo ulilojihusisha nalo.



- ❏ kuwaendea Waganga wa kienyeji
- ❏ Kuwasiliana na wafu
- ❏ Kuwaendea wapiga Ramuli
- ❏ Kutumia hirizi ili kupata nguvu zilizofichika(za kichawi)
- ❏ Kuangalia filamu za mashetani na kazi zake
- ❏ n.k. ________________

________________

________________

________________

________________

________________



Kama umeona ya kuwa umewahi kujihusisha na moja wapo ya hayo katika orodha hiyo hapo juu, unahitaji kuomba,ukikemea na kuyakataa matendo hayo katika jina la Yesu. Muombe mchungaji wako akusaidie zaid.




7. Tuko katika vita dhidi ya kweli na uongo, ambapo vita hushindwa katika ufahamu wetu. Ndiyo maana Yesu akasema "Mtaijua ________________ nayo kweli ________________," Yohana 8:32

8. Je, ni rahisi kuijua kweli? Kwa namna gani? ________________________

________________________________________________

9. Shetani mwenyewe hujigeuza awe kama ________________ na watumishi wake ________________________________ (2 Wakor.11:14-15). Dini za uongo na falsafa ni mifano ya mbinu zinazotumika. Watenda kazi wazuri sana wa shetani mara nyingi ni watu wazuri

10. Ufunuo 12:10b,inataja moja ya mbinu nyingine ya shetani. Ni ipi? ________

________________________________________________

Kwa nini hivyo ya kwamba,wakristo wengi hata baada ya kukiri dhambi zao bado huendelea kujisikia kuwa wenye hatia? Je , labda inawezekana kuwa huwa wanasikiliza sana mashitaka ya Shetani badala ya ahadi ya msamaha katika 1 Yohana 1:9?

11. Ahadi katika 1 Yohana 1:9 ni ipi? ________________________

Je, katika kifungu hiki Mungu ameonyesha ya kuwa kuna dhambi zingine ambazo ni kubwa na Mungu hawezi kuzisamehe? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

Je ni muhimu "kutubu" ili kusamehewa dhambi? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

Shida kwa Wakristo wengi ni kwamba huwa wanakataa kuupokea msamaha ambao Mungu hutoa. Badala yake wao huendelea kutubu na kutubu kitu kilekile kila leo. Wanasahau ya kuwa msamaha ni zawadi toka kwa Mungu. Kwa njia hiyo Shatani anapata ushindi kirahisi sana.

12. Efeso 2:2 inazungumzia watu wanaofuata ________________ na kwa kumfuata________________________mfalme wa uwezo wa anga.

Mtawala wa ufalme wa Anga ni Shetani anayetutia katika majaribu, akitumia vyote ambavyo Ulimwengu hutoa. Itakumbukwa kuwa dhambi karibu mara zote huwa ni ya kuvutia sana, hasa pale mwanzo.

**UJASIRI WA WAUMINI**

13. Ingawaje shetani hujaribu kututawala, sisi si wake. Soma Wakolosai 2:15. Kristo amefanya nini na nguvu za mapepo(nguvu na mamlaka)?

________________________________________________

14. Je, ni kwa jinsi gani 1 Yohana 4:4 inatupa ujasiri katika vita? __________

________________________________________________

15. Yakobo 4:7 inaahidi ya kuwa Shetani atatukimbia, lakini inatupasa kwanza ________________ Mungu na ________________ Shetani.

16. Soma 2 Wakor10:3-5 Je, kuna ushindi katika Kristo wa kuangusha ngome za Shetani? ________ inatupasa kufanya nini? Mstari 5b ____________

________________________________________________

Jadili kuwa ina maana gani kuyachukua mawazo yetu na utii wetu kwa Kristo.

## Hatua ya 6

# Silaha za Mungu



Mkristo hapaswi kukaa bila silaha katika vita vyake, kuna vyanzo vingi sana vya silaha, mojawapo ya Silaha za Mungu zilizotajwa katika Efeso 6:11-17.

| |
|---|
| Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S) |
| ____ Biblia ni sehemu muhimu ya silaha zangu. |
| ____ Imani ni kuamini ya kuwa Mungu anafanya yale aliyoahidi. |
| ____ Shetani hujaribu sana kutupotosha juu ya nafasi yetu katika Kristo. |

1. Ni nini makusudi ya silaha zilizotajwa katika Waefeso 6:11;13?_________

   _______________________________________________




***"Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani."(Mstari 14) "Tena ipokeeni chepeo ya wokovu na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu" (Mstari 17).***

Tumejifunza katika somo lililopita yakuwa Shetani hutumia uongo ili kuubadili ukweli kiasi cha kutunasa katika mitego yake.

2. Kitu gani kinachowaruhusu waumini kuwa huru? Yohana 8:32 _________

3. Kweli yaweza kupatikana wapi? Yohana 17:17 ______________________
   Ili mhasibu wa benki aweze kuitambua hundi bandia ni lazima awe anaijua hundi halali inafafanaje. Kwa kuwa si rahisi kuzijua fedha zote za bandia ambazo ziko, basi kuzijua vyema fedha halali kutakusaidia fedha bandia.

4. Ili kuwa na kweli "imefungwa viunoni mwenu," ni lazima kila mwamini awe na elimu ya kutosha juu ya kweli ya Kibiblia. Ni kwa jinsi gani mwamini anaweza kuongeza ufahamu wake juu ya Biblia? ____________

   _______________________________________________

| |
|---|
| Weka alama katika Jedwali jambo ambalo linaelezea vizuri hali yako |
| Ni kwa mara ngapi huwa ukisoma Biblia yako wakati wa ibada? |
| ❏ Kila siku ❏ Mara mojamoja ❏ Ni kama sifanyi |
| Je, huwa unakariri na kuvitafakari vifungu katika Biblia? |
| ❏ Mara kwa mara ❏ Mara mojamoja ❏ Ni kama sifanyi |
| Je,ni kwa kiasi gani huwa unasikia neno la Mungu likihubiriwa kanisani? |
| ❏ Kila juma ❏ Mara mojamoja ❏ Ni kama hakuna |
| Kwenye mzani wa 1-10, Jitathimini mwenyewe juu ya uwezo wako wa kuutambua uongo na madanganyo ya Shetani: |
| 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 |

5. Upanga wa Roho ni mzuri katika kushambulia na katika kujikinga pia. Je, ni kwa jinsi gani Waebrania 4:12 inaielezea Biblia?___________________

   _______________________________________________

   Tunapoihubiri injili tunakuwa tunavamia himaya ya Shetani. Tunafundisha Biblia na wala si mawazo yetu, kwa sababu Neno ndilo hupenya hadi ndani ya utu wa mwenye dhambi, likiwashawisha waikimbie dhambi.

6. Ili kweli ukulinde, ni muhimu kuwa _______________ pekee bali pia tuwe ____________________. Yakobo 1:22

**JAMBO LA KUTAFAKARI**



Efeso 6:16 Inatueleza kutumia ngao ya imani katika kuipinga mishale ya moto ya yule mwovu.
Orodhesha baadhi ya mishale ambayo Shetani amekuwa akitupiga nayo hivi karibuni

______________________
______________________
______________________
______________________
______________________

Je, ungemwambiaje mtu anayesema: "lakini sina imani ya kutosha.Imani yangu ni dhaifu."

______________________
______________________
______________________
______________________
______________________




Je twaweza kufanya nini ili kusaidia imani yako ikue

______________________
______________________
______________________
______________________
______________________




**"Dirii ya haki" Mstari 14**.

7. Kulingana na Warumi 3:24 tume ______________________ bure kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu. "Kupata haki" ina maana ya kuhesabiwa haki na Mungu; si kwa sababu tunastahili kuitwa wenye haki, lakini ni kwa sababu tunapompokea Kristo, anafuta deni la dhmbi zote tunazoshitakiwa kwazo.

8. Warumi 5:1 Moja ya matokeo ya kuhesabiwa haki na tuwe ______________________ kwa Mungu. Kwa kulitambua hili linatufanya kuondokana na uongo wa Ibilisi ya kuwa Mungu bado ametunza dhambi zetu tulizofanya katika vichwa vyetu,na kujua hakika tumesamehewa kabisa.

9. Kwa kuwa haki hutupa uhuru wa kuipinga dhambi, Sisi ni akina nani sasa? Warumi 6:18 ______________________________________________

   Kusema "Hapana" kwa dhambi na kufanyia mazoezi matendo ya haki ni ngao nzuri sana ya kuishinda dhambi?

   Kuvaa dirii ya haki ina maana ya kukumbuka kila siku ya kuwa hatuko katika hukumu tena. Hii inatulinda na mashitaka ya Shetani na na kututaka kuchagua haki badala ya uovu.

**UCHIMBUZI WA KINA**

Kulingana na Wafilipi 4:6-7 mkristo atakuwa katika amani iwapo atafanya kile mstari wa sita unatuambia tufanye.

____________________, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba,pamoja na kushukuru,

_________________________

Kila mmoja wetu inampasa kuchagua aidha amani au wasiwasi na msahaka.Wewe unachagua nini?

- ❏ Kuwa katika maisha ya amani, na kuyaacha mashaka yangu mikononi mwa Mungu.
- ❏ Kuwa na mashaka, kuubeba mzigo wa matatizo yangu mimi mwenyewe.




**"Na kufungiwa miguu utayari tupatao Kwa injili ya amani" Mstari 15**.

Kwa kuwa tuna amani Kwa Mungu (Warumi 5:1), inatupasa kuwa tayari siku zote kuipeleka injili ya amani Kwa watu wengine.

10. Warumi 10:15 inasema: "Ni mizuri kama nini ______________ ya hao ____________________," Kumbuka silaha tunayotumia katika kuihubiri injili ya amani ni upanga wa Roho, Neno la Mungu. Tuyaamini maneno yake, wala si maneno yetu au uwezo wetu katika kuigusa mioyo ya watu.




**"Ngao ya imani" Mstari 16**

Kutumia ngao ya imani, ni kuamini ya kuwa Mungu hutenda kama alivyo na kulingana na ahadi zake. Imani ni kuamini yale Biblia isemayo na kutenda sawa sawa.

11. Mishale ya moto ya yule mwovu ni ipi? Toa mifano __________________

    ______________________________________________________________




**"Kofia ya Wokovu" Mstari 17.**

Kofia hii ya chuma hulinda kichwa Kwa kuwa kanuni ya mashambulizi ya Shetani ni ufahamu wetu. Yeye Kama "Mshitaki" wetu hujaribu kutupotosha katika ufahamu wetu na kujaribu kutushawishi ili tujione ya kuwa tu wanyonge, tulioshindwa tusio na msaada. Lengo lake ni kutushawishi ya kuwa kamwe hatuwezi kuwa washindi, ya kwamba hata tunapojaribu kuyashinda majaribu ni kazi bure. Kumbuka katika Kristo sisi ni "Washindi", sio "washindwaji" (Warumi 8: 37-39)

12. Kuokoka kunaleta maisha mapya yenye faida nyingi kama vile:-

    Haki ya kuitwa ________________________________ Yohana 1:12

    Sitapotea kwa kuwa ni nao ______________________ Yohana 3:16

    Tuko na ___________________________ kwa Mungu. Warumi 5:1

    Dhambi zangu ____________________________. Wakolosai 1:14

**KUWA IMARA**

**Soma Mathayo 15-21 Juma hili (sura moja Kwa siku)**



***Kariri Waefeso 6:11***

***"Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuzipinga hilka zote za Shetani"***




### Hatua ya 7
# Samehe uwe huru

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Ni haki yangu kutowasamehe walionikosea.
____ Kusamehe kuna maana ya kusahau ulichotendewa
____ Naweza kupata uhuru kutokana na machungu kwa njia ya kusamehe pekee.

**HITAJI LA KUSAMEHE WENGINE**

Tafuta majibu ya maswali yafuatayo kutoka katika kitabu cha Waefeso 4……

1. Paulo aliwahimiza waumini kuishi kwa Unyenyekevu, wakichukuliana kwa upendo. Je, mimi leo ni kitu gani kinachotambulisha mahusiano yangu na wengin______________________________ Efeso 4:2

2. Je ina maana gani kuchukuliana ninyi kwa ninyi kwa upendo? Mstari 2.
______________________________________________

3. Kwenda kulala ukiwa na hasira maana utakuwa umempa njia ________ ____________________ Ef.4:26-27

4. Kwa nini si afya kwenda kulala ukiwa umejawa na hasira? __________
______________________________________________

   Katika vifungu vingine Paulo alizungumza juu ya umuhimu wa kusamehe ili Ibilisi asije akapata nafasi ya kutushinda (2 Wakorintho 2:10-11)

5. Fikiri kwa Muda. Ni kwa njia zipi Ibilisi anaweza kujitwalie ushindi ikiwa tutaiacha hasira ututawale? ______________________________
______________________________________________

   - Je, naweza kuwa huru hata kama sijawasamehe wengine? _________
   - Je, inawezekana kwamba naweza kuwa mtumwa wa hasira? ______
   - Je, naweza kuwa na amani na Mungu na huku namchukia ndugu yangu? ____________
   - Ni nani anayepata shida zaidi nisiposamehe? ❑ Ni Mimi ❑ Aliyeniudhi

**KUWA MTUMWA WA UCHUNGU/HASIRA**

Wakristo wengi wanaikataa amri ya kibiblia ya kusamehe,na wanachagua kuwa na fitina na wale waliowakosea. Wanapendelea kulipiza kisasi badala ya msamaha. Hata hudiriki kusema:-

*"Kamwe sitawasamehe kwa kile walichonitendea. Hapana nitawasamehe vipi kwa hayo waliyonitendea, nataka nione wakipata taabu."*

Wanashindwa kujua ya kuwa wao ndio watakaopata taabu kuliko. Wanapo-kataa kusamehe wanajikuta wamefungwa katika nyavu za uchungu/Hasira. Wanajikuta wamekuwa watumwa wa chuki na wenye shauku kubwa ya kisasi. Kamwe watu kama hawa hawawezi kuwa na amani na hiyo hali inaharibu mahusiano yao na watu wengi na hata na Mungu pia. Haijalishi kwamba huyo mwingine hata kama hasitahili kusamehewa. Njia pekee ya kuwa huru ni kuitii sheria ya Mungu ya kuwasamehe wale waliowakosea.




**MSAMAHA UKOJE NA SI KITU GANI**

Ina maana gani kumsamehe mwingine? Baada ya kusoma aya zifuatazo andika katika karatasi mawazo ambayo ni potofu ambayo uliwahi kusikia.

- Haina maana ya kusahau jambo ulilotendewa. Je isingelikuwa bora kufuta mara moja kumbukumbu hizo? Huchukua muda kwa kumbukumbu kufutika.
- Haina maana ya kuwaacha wengine waendelee kutuudhi na kunena mabaya juu yetu. Inatupasa kuwakemea au kuwaonya kwa upendo na kusema ingawaje nimekusamehe, lakini sitabaki na kinyongo juu yako.
- Ina maana ya kufanya maamuzi ya kuacha kuyashikilia. Ina maana kuacha mara moja kuendelea kuona picha ya namna vile walivyotukosea ndani ya ufahamu wetu. Kusamehe ni kukataa kutafuta namna ya kulipiza kisasi, na kuwaacha mikononi mwa Mungu, na kumwacha Bwana ashughulike nao.
- Ina maana ya kuishi na majuto ya dhambi za watu wengine. Hata kama hatupendi au tunapenda, tunapaswa kutambua ya kuwa tumeumizwa sana. Kukataa ya kuwa hatujaumizwa au kuwalaumu wengine haitamaliza tatizo. Jambo la msingi ni kutambua ya kuwa tumejeruhika na kujifunza namna ya kuishi na maumivu na kutafuta kupona. Kipi ni bora kubaki na uchungu au kusamehe?
- Tujiulize sisi wenyewe, Je, tunapenda kuwa watu wa hasira? Kama sivyo, msahama ndiyo barabara ielekeayo katika uhuru na amani.

KUWA IMARA



**Soma Mathayo 22-28 Juma hili, sura moja kwa siku**

***Kariri Wakolosai 3:13***

***"Mkichukuliana na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi vivyo hivyo ninyi."***

6. Tumehimizwa katika mstari wa 31 kuachana na uchungu, hasira, kelele na matukano. Ni nini mbadala wa hasira? Mstari wa 32 ____________________

**JINSI YA KUSAMEHE WENGINE**

7. Ni nani aliye mfano wa msamaha? Msatri 32 ____________________________

8. Msamaha wa Mungu ukoje? Ni watu wa namna gani ambao husamehewa na Mungu? Warumi 5:8 ______________________________________________

Soma Warumi 12:18-21 na jibu maswali yafuatayo:

9. Je, Inawezekana mara zote kuwa na amani na watu? Mstari 18 ___________

Kwa nini? ____________________________________________________

Wakati ambao siwezi kuwalazimisha watu wengine kuwa na amani na mimi, bado mimi naweza kuchagua kuwa na amani na wao. Ninaweza kufanya sehemu yangu kuwasamehe na kuwaomba msamaha niliowakosea. Nikifanya hivyo nakua huru haijalishi watasema nini au wataamua nini.

10. Kulingana na mstari wa 19, kwa nini hatupaswi kutafuta kulipiza kisasi? ______________________________

_____________________________________________________________________________

Je, wale wanaowaudhi wengine wataikwepa hukumu? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

Je, Mungu atawashughulikia siku moja? ❏ Ndiyo ❏ Hapana



11. Je nitashughulikiaje uovu? Mstari 21 ____________________________________________________________

12. Je, Nitaushindaje Ubaya kwa wema? Mstari 20 _____________________________________________________

Usemi "kuwapalia makaa ya moto kichwani" ina maana ya ukweli kwamba maadui zetu wanadhalilika sana tunapowatendea mema badala ya mabaya. Maana si tarajio lao ni kama mshangao kwao. Na hata wanashindwa kujua cha kufanya.

13. Je, kuna kikomo cha msamaha? Kulingana na Mathayo 18:21-22, ni mara ngapi inanipasa kumsamehe ndugu yangu? ____________________________________Ina maana gani? Je, kuna wakati ambao ni ngumu au haiwezekani au si muhimu kusamehe? ______________________________________________________

**HATUA KUELEKEA MSAMAHA**



1. Unajisikiaje kuhusu wale waliokukwaza? Ishinde hasira na uchungu wako. Ukishindwa kuitambua hisia yako yenye nguvu haitakuwa rahisi kuyafutilia mbali makosa waliyokukosea ili kuwapa msamaha.
2. Kumbuka kuwa Kristo alikufa kwa ajili yao kama alivyofanya kwako pia. Inawezekana hata hawastahili kusamehewa, je wewe haukusamehewa Kristo alipokufa kwa ajili ya dhambi zako.
3. Amua kuwasamehe hata kama haujisikii kufanya hivyo.Ingawaje myo wako wasema "Usiwasamehe", amua tu kusamehe,na kuiruhusu hasira yako iondoke.Maamuzi ni yako kama unataka kuwa huru na mambo yako yaliyopita.
4. Mwombe Mungu: "Bwana ninamsamehe ___________________________ (jina) kwa _______________________ ___________________________________________________________________________ (kosa alilokutendea)
5. Amua kutafuta mahusiano na wao kwa siku za usoni. Acha kuwashitaki!
6. Kumbuka kuwa kusamehe si kusahau. Si rahisi kufuta mara moja kumbukumbu kichwani, lakini tunaweza kuchagua kutafakari juu ya mambo mengine (mfano, Maandiko) kila mara mawazo ya kukumbuka mambo hayo yanapotuijia. Tunaweza hata kujikumbusha sisi wenyewe ya kuwa tayari tumekwisha wasamehe hao waliotukosea.
7. Usitarajie ya kuwa msamaha wako utaleta mabadiliko makubwa katika maisha ya huyo mtu. Haijalishi watajibu nini, lakini wewe umekwisha kusamehe songa mbele.

**Sasa! Maamuzi yangu ni yapi?** ❏ Nitasamehe ❏ Hapana, nitasubiri kidogo.



## Hatua ya 8
# Nisamehe

Jibu KWELI (K) au SI KWELI(S)
____ Unaweza kumpenda Mungu na kumchukia adui wakati huo huo .
____ Ni Munhimu sana kuomba msamaha kwa kosa ulilotenda hata kama mtu huyo hayuko tayari kukusamehe.
____ Ni bora zaidi kutafuta suluhisho kwa kuogea uso kwa uso na yule uliyemkosea.

Wakati mzozo unapotokea katika familia yako na umemkwaza mtu, Utafanya nini?

- ❏ Najisikia vibaya lakini sisemi jambo lolote kwao.
- ❏ Tunaacha kuongeleshana kwa muda. Na mwishowe tunaanza kuongeleshana tena, na tunajifanya mambo yamekwisha.
- ❏ Nawaendea, nasema nilchokosa na kuwaomba wanisamehe.

**KWA NINI UWAOMBE WENGINE MSAMAHA?**

1. Je, unapowapenda watu huwa unawadhalilisha na kuwakwasa ?________
   Je, unawatendeaje? ________________________________________
2. Soma 1 Yohana 4:20. Inawezekana kumpenda Mungu na kumchukia mtu mwinge wakati huo huo? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

Soma Mathayo 5:23-26 na jibu maswali yafuatayo.



3. Kama umemkwaza mtu nab ado haujatafuta suluhisho la tatizo, je ni rahisi kuwa katika ushirika na Mungu? ❏ Ndiyo ❏ Hapana
4. Je, sadaka yako, kuabudu au huduma yako kwa Mungu vitakubaliwa kama haujapatana na ndugu yako? Mstari 23-24 ❏ Ndiyo ❏ Hapana
   Kwa nini? ________________________________________
5. Kulingana na mstari wa 25, Kwa nini upatane na mshitaki wako haraka?
   ________________________________________
6. Ingawaje mashitaka mengi huwa hayafiki katika hatua ya sheria, je unafikiri ni busara kutatua kila shitaka mara moja linapotokea?
   ❏ Ndiyo ❏ Hapana Kwa nini? ______________________________
   ________________________________________

   Kulingana na mstari 22, tunapowaonea watu hasira watu hasira, tunawaweka katika hatari ya hukumu. Kushindwa kwetu kutafuta suluhisho kunamadhara kwetu sisi pamaoja na washitaki wetu.

   “Kama ndugu yako ana Neno nawe” katika kifungu cha 23, ina maana ya kuwa umefanya jambo la kumkosea. Ufungua wa kutafuta suluhisho ni kuwaendea, na kusema makosa yetu na kuomba msamaha.
7. Kwa nini unafikiri ni vigumu kumwendea mtu na kumwomba msamaha?
   ________________________________________

**UNAFIKIRI NINI?**

Utawajibuje wale wanaosema yafuatayo?

- Nitakuwa tayari kumsamehe kama atakubali kuliona kosa lake na kuibeba aibu.
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
- Ni bora nisikubali na kukiri kosa wala kuomba msamaha maana hali hiyo inaweza kutumiwa baadaye dhidi yangu.
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
- Kama nikimwomba msamaha atanicheka.
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
- Nilimwomba lakini hakunisamehe. Kwa hiyo kufanya hivyo kulinisaidia nini? Bado tuko kule tulikokuwa.
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________
  ______________________

**TAFAKARI JUU YA HILI**

Unafikiri ina maana gani kupatana na mtu mwingine au kupata suluhu?

___________________________

___________________________

___________________________

___________________________

Je, unahitaji kupatana na mtu? Nani?

❏ Mke
❏ Watoto
❏ Wazazi
❏ Majirani
❏ Marafiki
❏ Wengine.

___________________________

___________________________

Utafanya nini leo ili kuondoa ugonvi uliopo kati yako na huyo ili kuleta mahusiano ya karibu?

___________________________

___________________________

___________________________

___________________________



**KUWA IMARA**

**Soma I Kor.1-7,**
**Juma hili soma sura moja)**

***Kariri Mathayo 5:23-24***

***"Basi ukileta sadaka yako madhabahuni,na huku ukikumbuka kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yak, kisha urudi uitoe sadaka yako."***

## JINSI YA KUWAOMBA WENGINE MSAMAHA.

8. Kuna wakati ambapo maneno matupu hayatoshi. Wakati mwingine ni vizuri kufanya marekebisho ya mahali palipo haribiwa na wengine. Zakayo alikuwa mtoza ushuru, afisa dhalimu aliyewaibia watu vya kutosha. Alipookolewa aliahidi kufanya nini? Luka 19:8

____________________________________________________________

Wakati wa Agano la kale ilikuwa muhimu kulipa hasara uliyoisababisha pamoja na adhabu ya asilimia 20% (Hesabu 5:7). Ingawaje hatuishi chini ya sheria, kanuni ya kulipa fidia bado inafanya kazi hata leo.



**Kuomba msamaha ni mchakato unaopitia hatua mbalimbali.**

**Jiandae Kwa ajili ya kupatana.**

- Tambua ya kuwa ulikuwa katika makosa. Uwe mkweli. Tambua jambo ulilomtendea mwingine.
- Mara unapotambua kuwa ulikuwa na makosa, mwombe Mungu akusamehe.
- Kama yule mwingine pia anamakosa aliyokukosea, je wewe umekwisha kumsamehe?
- Tafuta mahali na wakati mwafaka wa kuongea na huyo mtu aliyekukosea au uliyemkosea.

**Wakati unapozungumza na mtu uliyemkosea.**

- Zungumza ana kwa ana, uso kwa uso ukiwa peke yako, isipokuwa katika hali ya jinsia hapo unaweza kulazimika kuwa na mtu mwingine. Katika hali kama hii ni muhimu mchungaji wako au mtu ambaye ni kama mshauri wako awepo.
- Tafakari maneno utakayotumia katika kuomba msamaha. lazima ulione kosa lako. Tumia kauli kama' "ilikuwa ni kosa", "na ninakosa" usijaribu kujifagilia au kujiosha.
- Uwe mnyenyekevu. Usijaribu kuyatetea matendo yako, au kumlaumu mwingine ili kujisafishia njia. Uyakubali makosa yako hata kama na yule mwingine ana makosa.
- Si rahisi kuingia katika kila kipengele, lakini lazima uwe wazi juu ya kusa unalotubu.
- Maliza kutubu kwako na swali la moja kwa moja. Je utanisamehe?
- Usiandike barua isipokuwa kama hakuna njia nyingine kabisa. Barua inaweza isieleweke vizuri au ikasomwa na watu ambao hata haiwahusu hata kidogo, nao wataanza kukusema kwa kejeli nawe ukajisikia vibaya.
- Inapowezekana lipa gharama kama umeharibu kitu.

**Je, itakuwaje Kama mtu hayuko tayari kukusamehe?**

- Mpe Mungu na uliache mikononi mwa Mungu. Wewe utakuwa umefanya sehemu yako, utakuwa uko huru hata kama yule mtu kakataa kukusamehe. Wakati mwingine itamchukua muda, mtu kukusamehe. Tafakari Warumi 12:18

9. Maamuzi yako ni yapi? Je, uko tayari kwenda na kumwomba msamaha yule uliyemkosea? ❏ Ndiyo ❏ Hapana
Anza leo kuufuata mchakato ulio elezewa hapo juu.



## Hatua ya 9

# Tumeitwa kuwa Watakatifu

Jibu Ndiyo (N) au Siyo (S)
____ Naweza nikaishi maisha matakatifu naya dhambi kwa wakati mmoja
____ Mungu anataka mimi niwe mtakatifu sababu yeye ni mtakatifu.
____ Ili kuwa mtu mtakatifunatakiwa kutenda matendo matakatifu

**TUMEITWA KUWA WATAKATIFU**

Marakwa mara mtume Paulo aliwaita waaminio kuwa "watakatifu" (Waefes.1:1, Wafilipi 1:1). Kwanini? Aliwaita hivyo kwa sababu inawaelezea wao ni kinanini katika kristo. Kwasababu ya damu ya Yesu, wamekuwa watakatifu na wenye haki.

1. Katika 1 Wakorintho 1:2, Kristo ametutakasa hii inamaana ametutenga kuwa watakatifu. Ingawa tayari tumetakaswa, tumeitwa kuwa?

   Mstari 2 ______________________________. Hii inamaanisha kwamba Mungu anatuhitaji tuache dhambi na kuishi maisha ya Kumpendeza yeye.

2. Takatifu ninini? Tunaweza kuelezea kama ifuatavyo:
   - Ina maana kuacha dhambi na kujitoa kwa Mungu.
   - Ni moja ya tabia za Mungu, ndivyo alivyo. (1 Petro 1:15-16)
   - Ni kitu amabcho tunaweza kukipata toka kwake. (2 Kort 7:1, 1 Theso 4:3)

3. Soma 1 Petro 1:15-16 jibu mtakatifu ni nani? ________________________
   Naweza kuwa mtakatifu? ❑ Ndiyo ❑ Hapana

   Baadhi wanafikiri watu kama sisi hatuwezi kuwa watakatifu. Je, mungu anaweza kutuagiza kitu ambacho hatuwezi kutimiza? Hii haimaanishi kuwa tutakuwa wakamilifu, lakini tunajitahidi Kutimiza lengo kwa kujitenga na dhambi

4. Kwanini wakristo wengi hawaishi katika utakatifu? Bibilia yatwambiak-wamba kuwa mtakatifu, ni lazima kuacha vitu fulani.

   Mfano, 1 Wathesalonike 4:3, 7, inasema ni lazima kuacha:

   ________________________ (Mst.3) na ________________________ (Mst.7)
   Orodhesha mambo mengine ambayo Roho mtakatifu anataka uyaache:

   ________________________________________________________________

5. Hivyo basi, Jinsi gani utakatifu ni muhimu katika maisha ya Kikiristu? Je ni uchaguzi au ni lazima? ______________________________________________

**TUNAWEZAJE KUISHI KATIKA UTAKATIFU?**

6. Kukua katika utakatifu ni lazima________________________________________

   ___________________ 2 Wakorintho 7:1 Unaweza kufikiri mfano wowote?

7. Mungu alifanya nini kutusaidia sisi kuishi maisha yaliyo safi? 1 Yohana 1:9

   ________________________________________________________________

8. Soma Mithali 4:23 Tunatakiwa kulinda nini? ___________________________

**FIKIRI JUU YA HILI**

"Piga mbio namna hiyo ili upate tuzo" 1Kor 9:24



Maisha yako ya sasa yatakusaidia kupata tuzo?
- ❑ Ndiyo
- ❑ Hapana
- ❑ Sina hakika

Kama huna uhakika, jaribio lifuatalo linaweza kukusaidia kugundua ni kwanini.

**ANGALIA MUDA**

Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuzuia ukuaji wako. Angalia mambo yafuatayo kutoka katika orodha ambayo unadhani yanakuweka mbali na maisha ya kiungu

- ❑ Marafiki
- ❑ Familia
- ❑ Kazi
- ❑ Muziki
- ❑ Luninga, mtandao, n.k.
- ❑ Mali
- ❑ Kutokujitoa kwa Mungu
- ❑ Shughuli za kila siku
- ❑ Kutokjumuika pamoja na wakristo wenzako( katika vikundi vidogovidogo, kanisani, nk)
- ❑ Tabia, kama zipi?

  ______________________

  ______________________

- ❑ Uko tayari kufanya mabadi-liko ya lazima, kutubu na kuacha dhambi zako?

  ______________________

  ______________________

**CHIMBA NDANI ZAIDI**

- Utakatifu unaanza katika kile tunachofikiri na kukua katika vitendo vitokavanyo na kile tuanchofikiri. Wafilipi 4:8
- Utakatifu ni pamoja nakuzuia mwili tamaa pamoja na hisia. 1 Wakorintho 9:27

**NITAWEZAJE KUSIMAMA**

*Mungu amenipa kila kitu kinnipasacho kuishi kitakatifu*

- Aliniokoa mimi
- Alinitoa katika kifungo cha dhambi
- Niko huru mbali na hukumu
- Roho mtakaifu anaishi Ndani yangu nipate kuzaa matunda
- Amenipa biblia ili inifundishe namna ya kuishi
- Amenipa nafasi kuyatoa maisha yangu kwake



**KUONGEZEKA NGUVU**

**Wiki hii Soma**
**1 Wakorintho 8-14**
**Sura moja kila siku**

***Kariri 1 Petro 1:14-15***

***"Kama watoto wakutii msijifananishe Na tamaa zenu za kwanza, Bali Kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, hivyo iweni watakatifukatika mwenendo wenu"***

9. Biblia inatupa ushauri gani juu ya kilinda moyo wako?

   Zaburi 119: 11 ______________________________

   Wakolosai 3:2 ______________________________

10. Warumi 6:19 inasema nini kuhusu kuishi maisha ya haki? __________

    ______________________________

    Kama tulivitoa viungo vyete katika uchafu, basi tuvitoe Kwa Mungu, tuwe watumwa WA haki na sio wa dhambi.

**KUJITOA KWA KILA SIKU**

11 Soma Warumi 12:1-2 Mungu ananitaka nifanye nini? Mstari wa 1

______________________________

12. Dhabihu iliyo hai ni nini? ______________________________

    ______________________________

Maombi yafuatayo ni kielelezo cha dhabihu iliyo hai




*"Mungu ninajitoa kwako*
*Linda akili yangu na yote ninayo fikiri*
*Linda macho yangu na vyote nivionavyo*
*Linda masikio yangu na vyote nisikiavyo*
*Linda kinywa changu na vyote ninenavyo*
*Linda moyo wangu hisia zangu pamoja na mtizamo wangu*
*Linda mikono yangu na vyote nifanyavyo*
*Linda mguu yangu na kote niendako*
*Linda mwili wangu ni hekalu lako*
*Nijaze na roho wako mtakatifu*
*Ninapenda kukutii wewe*
*Napenda nifanye mapenzi yako"*

13. Toa mifano ya mawazo na matendo yasiyo ya kiafya katika dunia ya leo

    ______________________________

    ______________________________

14. Ili kutoifuatisha namna ya dunia hii, tunatakiwa kufanywa upya (Mstari 2) ______________ Hivyo tutajua Mungu anataka tufanye nini.

    Ni njia zipi zitatuwezesha kufanya upya nia zetu? ______________

    ______________________________

15. Maelezo haya yanatutaka kuyatoa maisha yetu ili kumpendeza Mungu, nakupokea baraka zake. Uko tayari kujitoa leo, nasiku zote za maisha yako? ❏ Ndiyo ❏ Hapana

    ______________________ Tareh __________

    Weka sahihi hapo juu kwa kumbukumbu ya kujitoa kwako.




# Hatua ya 10
# Uwakili

Jibu Ndiyo (N) au Siyo (S)
____ Kuna mambo muhimu zaidi ya kiapto kizuri na maisha mema
____ Wale tu wenye uwezo ndo watatakiwa kujitoa kanisani
____ Vitu vyote tulivyo navyo viimetoka kwa Mungu

**MSIMAMO WANGU KATIKA VITU**

1. Katika Luka 12:15, Kwa nini natakiwa kujilinda na choyo? ______________

   ______________________________________________

   Kama uzima wa mtu hautokani na vitu, kipi ni muhimu? Luka 12:31

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. Soma 1 Timotheo 6:17-19, kwa nini tunatakiwa tusitumaini utajiri?
   Mstari 17 ______________________________________

3. Nitapata wapi kile kinachohitajika ili niishi kwa furaha? Mst.17 _________

   Ni mara ngapi huwa natoa shukrani kwa Mungu? ____________________

4. Mkristo anatakiwa kutafuta wapi utajiri? Mstari 18-19 ________________

   ______________________________________________

   Utadumu kwa muda gani? _____________________________

5. Biblia inasema mimi ni mtumishi, na wakili mwema wa Mungu. Ili kuwa wakili mwema, nini kinahitajika? 1 Wakorintho 4:2 __________________

   ______________________________________________

6. Mungu ametupa vitu gani ili kuvitawala? ___________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

**KUZITAWALA PESA ZANGU**



Pesa ni kati ya vitu ambavyo Mungu amenipa ili nizitumie. Biblia inatufundisha kwamba ni muhimu kurudihsa kwa Mungukama sehemu ya vile vitu alivyotupa. Hivi vinaitwa sadaka na Zaka.

7. Ni wakati gani ninatakiwa kutoa Kwa Mungu? 1 Wakorintho 16:2
   ____________________________. Hii inamaanisha ni muhimu kusaidia kazi ya Mungu wakati wote, sio kwa muda. Fulani unaposikia kuna uhitaji. Siku ya kwanza ya juma inamaana ya Jumapili.

**KITU CHA KUFIKIRI**

Soma habari ya Eliya katika 1 Wafalme 17:8-16

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

Unafiukiri ni muhimu kujitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu? Kwanini?

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

Kristo ametoa tahadhali gani kwa watu wanaotegemea utajiri wao kama kinga na furaha yao? Luka 12:16-21

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

**HEBU FIKIRI NA KUAMUA**

Nini pato langu kwa wiki/mwezi

___________________________

Ni nini moja ya kumi ya mapato yangu? (Zaka)

___________________________

Kanisa langu lazima liwe la kwanza kupokea msaada wangu, maana ndo ninakopata mafundisho na uangalizi.
Na zaidi, kuna miradi mingine ninaweza kusaidia kama huduma.

Kwa msaada wa Mungu ninatakiwa kusaidia kazi ya

Mungu kwa: _______________ kila mwezi



**KUWA IMARA**

**Wiki hii soma**
**1 Wakorintho 8-14,**
**(sura moja kila siku)**

***Kariri 2 Wakoritho 9:6***

***"kumbuka hili: Apandaye haba atavuna haba, na apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu"***

8. Je nisa hihi kutoa wakati tu tukiwa na zaidi? ❑ Ndiyo ❑ Hapana

   Kwanini? ________________________________________________

9. Tunatakiwa kuzingatia nini wakati tunapotaka nini cha kutoa?

   1 Wakorintho 16:2 ______________________________________
   Matoleo yetu yanatakiwa kuwa sawa na kipato chetu, wale wanaopata zaidi watoe zaidi. Wanaopata kidogo watoe kidogo.

10.Katika agano la kale, Zaka ilikuwa ni lazima.(Mambo ya Walawi 27:30-32)

   Zaka ni nini? ___________________________________________

   Zaka ni moja ya kumi ya kitu chochote. Yaani asilimia 10%

11. Kama wakati wa agano la kale walitoa sehemu ya kumi ya mapato yao kwa Mungu, sasa tuko katika Kristo, tusitoe angalau kiasi hiki?
   ❑ Ndiyo ❑ Hapana

## MTAZAMO WANGU KUHUSU UTOAJI

12. Katika 2 Wakorintho 9:6, sadaka zetu ni hazina kwa kazi ya Mungu,

   hivyo tunatakiwa kutoa ___________________________________

   Ingawa wakristo wa Makedonia walitoa Sadaka kwa Paulo kwaUkarimu (2 Wakorintho 8:1-3) wajibu wa kutoa kwa kazi ya Mungu sio kwa ajili ya matajili pekee.

13. Katika 2 Wakorintho 9:7 lazima tutoe kama ____________________
   Katika mioyo yetu. Hii inamaana, ni muhimu. Kupanga kile tunachotaka kutoa Kwa kazi ya. Mungu wala si Kwa kulazimishwa

14. Katika 2 Wakorintho 9:7 tunatakiwa kutoa "si kwa ________________

   au _________________ sababu Mungu anapenda ________________"

15. Tunatakiwa kuangalia nini? Matayo 6:1-2 ______________________

   ______________________________________________________

   Tunatakiwa kutoa namna gani? Matayo 6:3-4 __________________

   ______________________________________________________

## BARAKA ZA UTOAJI

16. Kifungu hiki kinatueleza nini juu ya baraka za Mungu kwa wanaotoa kwa ukarimu?

   2 Wakorintho 9:6 _______________________________________

   ______________________________________________________

   Matendo 20:35 _________________________________________

   ______________________________________________________

   Kwa nini kuna baraka katika kutoa kuliko kupokea?_______________

   ______________________________________________________






Hatua ya 11

# Ninaweza, lakini nifanye?

Jibu NDIYO au HAPANA
____ Biblia haizuii vitu ingawa sio vizuri kwangu
____ Matendo yangu yanaweza kuwa vikwazo vya kuzuia wengine
____ Uhuru wangu katika kristo unanipa ruhusa ya kufanya nipendacho

Waumini tofauti hufikiri tofauti kuhusu vitu vilivyomo katika jamii yetu. Mfano, kunamitizamo tofauti kuhusu kipi ni sahihi kuhusu mavazi, mziki pamoja na viburudisho kwa mkristo.

“Mashaka” haya yanaleta hofu kati ya wakristo kwa sababuwengine wanasema yanaruhusiwa na wengine wanasema hayaruhusiwi. wakati kukiwa na kutokukubalianakatika vitu Fulani, Biblia haijawa wazi ni kipi imezuia, hatupashwi kulaumiana endapo tutatofautiana.

Wakati wake, Paulo alialiweka sawa jambo la mkristo kula ama kuto kula nyama iliyotolea kwa miungu. Kanuni zifuatazo kutoka katika maandiko yake zitatusaidia kufanya maamuzi katika sehemu zenye “mashaka”

**JE INAFAA? INAJENGA?**

1. Katika 1Wakorintho 10:23 Paulo anatuonyesha kanuni muhimu zinazotusaidia katika maisha yetu. Anamaanisha ninikatika kifungu hiki ”vitu vyote ni halali, bali si vyote vifaavyo”? ____________________

   ____________________

2. unaweza kutoa mfano ambacho si kizuri kwako, hata kama hakijaelezwa katika Biblia? ____________________

   ____________________

3. Kwanini tuepuke baadhi ya vitu? Anaglia sehemu Mwisho ya 1 Wakorintho 10:23 kisha kamilisha kifuatacho: Ingawa ninauhuru wakufanya mambo mengi, ila sio vyote____________________

   Ni vyema kuepuka vitu visivyojenga, hata kama Biblia haijavizuia. Njia nzuri ya kuamua kama kitu kinafaa ni kujiuliza maswali yafuatayo:

   - *Je hili litanisaidia kukua kama mkristo?*
   - *Je litazuia kukua kwangu kwa namna yeyote?*

4. Soma 1 Wakoritho 6:12. Sehemu ya mwisho ya mstari inamaanisha nini?

   ____________________

   Maisha ya wakristo wengi yanatawaliwa mambo ya kisasa, muziki, kile wanachoona kwenye luninga n.k. mara kwa mara hawagundui au kukubali jinsi gani zina athili baadhi ya mambo katika maisha yao.

5. Kama kuna kitu kinaongoza maisha yako, je kinajenga? ____________
   Je kuna mambo ambayo yamekuwa kizuizi, yanatawala sehemu ya maisha yako? ____________, kama ndiyo, ni mambo gani hayo? ____________

   ____________________

**FIKIRI JUU YA HILI**

Chukua muda kufikiri juu ya maisha yako. Je matendo yako yanawajeka waumini wengine?

Orodhesha baadhi ya vitu ambavyo vinaweza vikasabaisha wengine kuanguka. Omba mungu akusaidie uweze kushinda sehemu hiyo kwa faida ya wengine.

____________________
____________________
____________________
____________________
____________________

Sasa fikiri ni njia gani ya kusaidia kuwajenga waumini wengine. Orodhesha mifano halisi hapa chini

____________________
____________________
____________________
____________________
____________________



**KWA KUJISOMEA ZAIDI**

Soma wakolosai 2:23-24 Orodhesha kanuni unazozipata humo.

____________________
____________________
____________________
____________________
____________________



**JAMBO LA KUFANYA**

Soma na tafakari juu ya 1 Wakorintho 10:2333, orodhesha vitu ambavyo vinafaa katika maisha yako.

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

**KUWA IMARA**



**Soma 2 Wakorintho 1-7 wiki hii (sura moja kila siku)**

***Kariri 1 Wakorintho 10:23***

***Vitu vyote ni halali bali si vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali bali si vyote vijengavyo.***

## JINSI GANI INAATHILI WENGINE, KANUNI YA UPENDO.

6. Tahadhali gani tunaipata katika 1 Wakoritho 8:9? ____________________
______________________________________________________________

7. 1 Wakoritho 8:13 inatupa msimamo wa Paulo kuhusu kuwa kikwazo kwa wengine? Uamuzi wake unatuonyesha nini? __________________________
______________________________________________________________

8. Mambo gani mawili mkristo anatakiwa kuyaepuka? Warumi 14:13
______________________________________________________________
______________________________________________________________

9. Ni vitu gani katika maisha yako vinaweza kuwa vikwazo kwa Wakristo wengine? ______________________________________________________

10. Jitahidi kwa _________________________ & ___________________ ______________________________________ Warumi 14:19

***"mtu asitafute faida yake mwenyewe bali ya mwenzake" 1 Wakorintho 10:24.***

Kufikiri juu ya wengine iwe kanuni ya kutuongoza maishani. Sasa kunamambo, na vitendo vingi ambavyo yanakubalika kwa baadhi ya watu, bali si kwa wengine. Kunaweza kukawa na vitu kama, mavazi, jinsi ya kuongea, vyakula, viburudisho hatavingine ndani ya kanisa. Kwahiyo basi, upendo utumike kuonyesha wapi mipaka ya wengine inaishia na wapi inaanza mipaka ya  wengine. Bila kujali wengine, nitajiwekea mipaka sehemu Fulani

## JE INAMTUKUZA MUNGU?

11. Nini liwe lengo kwa kila jambo nitendalo? 1 Wakoritho10:31 ___________
______________________________________________________________

Jiulize:  naweza kufanya jambo na kumtukuza Mungu wakati huohuo?



**Kwa ufupi**   Penye mashaka lazima nizingatie:

- Hatakama haijazuiwa, inafundisha? Inafaida?
- Inaathili vipi waumini wengine?
  Je inawajenga? Au inawawekea vikwazo?
- Inaleta utukufu kwa Mungu?

**EPUKA KUTOKUWA NA KIASI**

**KIBALI:** Baadhi ya wakristo wanatumia uhuru wa kikristo bila hekima, hawachunguzi yale wanayofanya jinsi yanavyo athili ukuaji wao. Pia hawajali jinsi gani matendo yao yanaathili wengine. Yaani hawajali huohuo, wanahukumu wengine ambao wanauhuru wa kufanya jambo Fulani. Mara nyingi wanaonyesha tabia ya kuwa juu, upinzani na kutokukubaliana.

**UHALALI:** Maisha ya waumini wengine yanaongozwa na sheria. Wanaamini kwamba kuishi kiroho ni kufuata sheria Fulani. Uelewa wao kuhusu ukristo umesimamia katika mambo yale amabayo hawatakiwi kufanya na si yale wanayotakiwa kufanya.wakati

**MAISHA MAKAMILIFU:** Mtu huyu anachunguza vitu vyenye mashaka, anaepuka vitu vyeney mazala au visivyo jenga. Katika upendo wa waumini, wanajizuaia kupitia uhuru wao, ili wasiwe kikwazo kwa wengine.wanatafuta kumpendeza Mungu katika kila walitendalo.




# Hatua ya 12
# Uamuzi

JIBU NDIYO (N) AU HAPANA (H)
____ Biblia ni kitu pekee kinachoongoza maisha yetu
____ Wahubiri wote wanahubiri kile kilichomo katika biblia
____ Ni muhimu kuisoma Biblia lakini sio kuitii

Tunauliza maswalihaya sababu ulimwengu tunaoishi ni mahari. Panapotuchan-gaya sana. Nani anayetuambia ukweli? Jinsi gani Nitafanya uamuzi wa busara?

## BIBLIA INATUONESHA NJIA SAHIHI

1. Katika ulimwengu ambao unatafuta ukweli, lini ukweli Utapatikana?
   ______________________________________________ Yohana 17:17

2. Kipi ni sahihi kusema? ❑ Biblia ina ukweli.
   ❑ Biblia ni ukweli.



3. Kujifunza biblia kunafaida gani katika maisha yetu?
   Zaburi 119:98 ______________________________________________
   Zaburi 119:130 ______________________________________________

4. Biblia ni kubwa, lakini tunatakiwa kuelewa nini Matayo 7:24-27 anasema.
   Wale ambao ____________ maneno ya Kristo na ____________________ atafananishwa na mtu mwenye Busara aliye jenga nyumba yake juu ya mwamba. Mstari 24
   Wale ambao ____________ maneno ya kristo na ____________________ Wanafananishwa na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba juu Ya mchanga. Mstari 26

5. Nini tofauti ya wanaojenga juu ya mwamba na wale wanao Jenga juu ya mchanga? ______________________________________________
   ______________________________________________

6. Katika Yohana 7:17, mtu atakayetofautisha ukweli na uongo Ni yule
   ______________________________________________

   Kutokana na kifungu hiki, haitoshi tu kujua nini Mungu anataka; ni lazima tuchague kufanya kile ambacho biblia. Inasema. Angalia pia katika Yakobo 1:22-24.



## JILINDE NA WALIMU WA UONGO

7. Kama mhubiri ni maalufu sana, inamaanisha kwamba mafundisho Yakle ni ya kibiblia? ❑ Ndiyo ❑ Hapana

8. Wahubiri wengi na walimu wanaonekana wazuri wakati wakiongea kuhusu Mungu, ingawa sio lazima waongee ukweli. Matayo 7:15 inatufundisha nini? ______________________________________________

**WAKATI WA KUAMUA**

Baada ya kusoma somo hili utagundua kwamba hapo mwanzo ulikosauamuzi wa kiroho.

Pengine umesikia ushauri usio wa busara, au pengine umehusika katika kanisa ambalo linnawaongoza waumini badala ya kuwaongoza wajifunze Biblia wao wenyewe. Au pengine umechukuliwa na mafundisho ya wahubiri bila kupima ujumbe wao.

Haijalishi ni sababu ipi,kama umegundua unahitaji uamuzi, utafanya nini juu ya hilo?

Kumbuka ulichojifunza katika somo la 6, ili kugundua Ankala ya uongo, mtu wa bank lazima ajue ankala ya ukweli ina fananaje. Sio rahisi kugundua kila aina ya fedha za udanganyifu, lakin kama najua ankala za ukweli, itakuwa rahisi kugundua iliyo ya uongo

Ili kuamua juu ya ukweli au uongo ni laziam kuifahamu biblia vizuri

❑ Leo nachagua kutumia muda wangu mwingi kujifunza maneno ya Mungu

❑ Naahidi kujitoa kila siku ____________ (muda)

Sahihi ____________________

Tarehe ____________________

9. Tutamtambuaje mtu wa Mungu kweli kweli? Mathayo 7:16-17

______________________________________________________________

10. 2 Timotheo 2:15 anatuambiaje kuhusu kutumia neno la Mungu? ______________________________. Sikuzote Kunakujalibiwa kubadili neno kulifanya lionekane Kama vile tunavyotakakusikia au kipi ni maarufu Angalia 1 Wathesalonike 2:3-6.

11. Kuna wahubiri wanopindisha neno la Mungu? ❑ Ndiyo ❑ Hapana

Tutawatambuaje? ______________________________________________

______________________________________________________________




**JINSI YA KUCHAGUA KANISA LINALOHUBIRI UKWELI**

Maswali yafuatayo yanaweza kulipima kanisa.

| | | |
|---|---|---|
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Ujumbe unaieleza biblia wazi na kwa mpangilio? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Viongozi wake ni watu wa Imani, wanaonyesha tunda la Roho? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Unaruhusiwa kufikiri wewe binafsi na sio kukubali tu kile kinachohubiriwa? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Je liko huru katika kujaribi kila roho? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Je waumini wake wanaonyesha kujali na huruma wao kwa wao? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Mafundisho ya Biblia yanachukua nafassi kuliko mihemuko? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Waumini wanahimizwa kujisomea Biblia wao wenyewe? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Je Kristo anainuliwa kuliko watumishi? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Je ujumbe unajenga zaidi kuliko kukemea? |
| ❑ Ndiyo | ❑ Hapana | Je Neema inasisitizwa kuliko sheria? |

## KUTAFASIRI BIBLIA



Kwa nini kunamchanganyiko mwingi katika tafasiri ya baadhi ya vifungu? Kanuni zifuatazo zitasaidia tafasiri sahihi Ya neno la Mungu.

- Maandiko yasomwe akili ikiwa wazi, zingatia kile roho mtakatifu anataka tujifunze. Tuweke kando mawazo binafsi na mapokeo.
- Tafasiri Biblia kama ilivyo, maneno, maneno yake yaeleweke katika hali ya kawaida kabisa na si kutafuta maana zilizofichika.
- Zingatia maana ya mstari unapojaribu kuutafasiri. Maana ya mstari inatokana na mistari iliyotangulia na inayofuata, pia na mazingira ulipoandikwa. Kutozingatia mazingira kutaharibu ukweli.
- Acha Biblia itoe tafasiri yenyewe kwa kulinganisha kifungu kimoja na kingine. Kifungu kigumu au kifungu kisichowazi, lazima kitafasiliwe kwa kuzingatia, kifungu kinachoeleweka, amabacho maana yake ipo wazi.
- Zingatia lugha za picha kama , sitiari, tashbihi na mlinganisho. Kwa mfano, Yesu anaposema "mimi nimi njia" anaongea kwa lugha ya picha.

**KUCHIMBA NDANI ZAIDI**

Nitajuaje Mapenzi ya Mungu juu ya maamuzi yangu katika maisha?

Angalia mwishoni kisa kisema-cho: kujua mapenzi ya Mungu

**KITU CHA KUFIKIRI**

Baadhi ya makanisa yameweka misingi ya imani yao katika mapokeo ,kuliko Biblia. Wakati mwingine mapokeo haya yana-haribu ukweli wa Biblia. Unaweza kufikiri juu baadhi ya mapokeo ya kidini ambayo yana-pungukiwa msaada wa kibiblia?

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________



**KUWA IMARA**

**Soma**
**2 Wakorintho 8-13**
**Na zaburi 17**
**(Sura moja kila siku)**

***Kariri 2 Timotheo 2:15***

***Jitahidi kujionyesha kuwa umekubalika mbele za Mungu, mtenda kazi asiye tahayari, akitumia halali neon la kweli.***



Hatua ya 13

# Kuwashirikisha habari za Kristo

Jibu Ndiyo au Hapana
____ Ni sawa kwangu kufanya uamuzi wa kupeleka au kutopeleka injili.
____ Watu wengi duniani wataenda mbinguni.
____ Mwinjilisti  wa kweli ni yule anayehurumia waliopotea.

**KWANINI TUHUBIRI  INJILI?**

1. Warumi 3:10-12,23 inasema nini kuhusu  hali ya ulimwengu? ____________
________________________________________________________________
Hakuna mtu aliyemwema kuweza kuingia mbinguni kwa uwezo Wake mwenyewe. Wote tunamhitaji Kristo.

2. Matayo 7:13-14 inaonglelea njia mbili zenye mwisho tofauti. Njia pana iendayo____________________; Njia nyemababamba iendayo ______________.
Nini itakuwa mwisho wa watu walio wengi?___________________________

3. Matayo 7:15.Moja ya sababu ya wengi kupotea  ni kwasababu Kuna __________________ wengi. Yesu aliwaita hawa walimu wa uongo, mbwa mwitu waiojivika ngozi ya kondoo, kuonyesha kwamba maranyingi mafundisho ya uongo huelezewa kama kitu kizuri au chenye kuvutia.

4. 1 Yohana 2:28 anatuambia tu _______________________ katika Kristo ili kwamba akija tuwe na ____________________ na si ____________________
Wale wakaao katika kristo wataii amri a krosto ya kupeleka injili ulimwenguni mwote. Hatujui siku wala saa, bali kila siku inatusogeza katika ujio wa Kristo. Warumi 13:11



5. Uinjilisti sio hiari kwa wakristo. Sio kitu cha kufanya mtu anapojisikia. Andika amri inayopatikana katika kifungu kifuatacho .

   Matayo 28:19 ____________________________________________________

   Matendo 1:8 _____________________________________________________

   2 Timotheo 4:2 ___________________________________________________

   Kama tunavyoweza kuona, uinjilist umeamrishwa na sio kitu cha kushauriwa. Ili kufikisha ujumbe sahihi, wakristo wanatakiwa kutimiza mambo Fulani.

**MAHITAJI YA UINJILISTI WENYE MATOKEO**

6. Yohana 3:3 Mwinjilisti anatakiwa ____________________________________

7. Katika Yohana 15:4-5 tunatakiwa _______________________ katika Kristo.
Hii inamaanisha kuishi katika ushirika nakumtegemea yeye.




**TAFAKARI**

Soma Ufunuo 20:11-15 kisha chagua moja kati ya yafuatayo

❏ Je unapenda familia yako au rafiki zako watupwe katika ziwa la moto?

❏ Ungependa kuwa nao pamoja katika maisha ya milele mbinguni? Ufunuo 21:1-7

**KITU CHA KUFANYA**

Kuanzia sasa ninajitoa kuomba juu ya watu wafuatao, nikimuomba Mungu anipe nafasi ya kuwaambia habari za Kristo.

______________________
______________________
______________________
______________________
______________________
______________________



**USHAURI KWA WALIO KATIKA IMANI MOJA**

1. Uwe mkweli. Wengine watajua kwamba unamaanisha kile unachokisema.
2. Angalia muonekano wako (Usafi binafsi, vaa vyema n.k)
3. Uwe mwenye huruma. Jinsi unavyosema ni muhimu kuliko kitu unachosema.
4. Uwe mpole. Lengo sio kushinda katika malumbano.
5. Sikiliza. Hii itakusaidia kufikisha injili kikamilifu.
6. Kariri mistari katika maandiko kusaidia ufikishaji wa injil.

**KITU KINGINE CHA KUFIKIRIA**

Andika mahitaji ya 1 Petro 3:15 kisha tafakari.

____________________________
____________________________
____________________________
____________________________
____________________________
____________________________

**KUWA IMARA**

**Soma 1 Timotheo 1-6 Na Zaburi18 wiki hii (sura moja kila siku)**



***Kariri Warumi 10:15***

***Watahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa "Jinsi gani ilivyo mizuri miguu yao wapelekao habari njema"***

8. Matayo 9:36, 14:14. tunatakiwa ________________________ kwa watu, kama jinsi kristo alivyofanya.

9. Katika Matayo 7:29 tunatakiwa kuongea kwa______________________. Hii haimaanishi kuwa tuzunguke tukifanya miujiza ya kuponya bali ujumbe wetu uwe ni wa kiroho. Biblia ni chombo chenye nguvu kinachoaminiwa kushawishi watu na mahitaji yao, zaidi ya yote maisha yetu yanatakiwa kuonyesha, Mungu amefanya nini katika maisha yetu. (Matayo 5:16)

10. 2 Timotheo 1:8 Hatutakiwi ________________________________________

## KAZI YA MUINJILISTI

**Omba:** Omba masaada wa Roho mtakatifu, ili kufikisha injili wakati muafaka
**Chunguza maandiko:** Kama mtumwa wa Mungu, ni muhimu Kusoma maandiko mara kwa mara. Hii inatupa ushahidi kuhusu Kristo. (Yohana5:39)

**Kariri mpango wa wokovu:** Angalia mpango rahisi wa wokovu ulioambatanishwa mwisho soma na kariri. Hii itakufanya kuwa tayari kushirikisha wengine habari za Yesu mara upatapo muda itakupa uhuru na ujasiri unaposhirikisha wengine.

## JINSI YA KUANZA MAZUNGUMZO YA KIINJILISTI



Tegemea roho wa Mungu afungue mlango wa kushuhudia. Maswali yafuatayo yatakusaidia kuanzisha mazungumzo.

- Fikiri kama ungekuwa umekufa leo Mungu anauliza: "kwanini nikuingize mbinguni"? Utajibu nini?

  Majibu yao yataonyesha kama kweli mtu alielewa injili au wanaamini wameokolewa kwa jitihada zao.
- Kwa maoni yako, mtu anatakiwa afanye nini ili afike mbinguni? Ungependa kujua Biblia inasema nini kuhusu hili?
- Mtu anapokueleza kuhusu matatizo yake, uliza: Naweza kukuombea sasa hivi? Watu wengi watashukuru kwa maombi yako. Hii pia itaacha mlango wa mazungumzo wazi kwa wakati mwingine.
- Unaweza kunipa maoni yako kuhusu kipeperushi hiki? Kama mtu akisema "ndiyo" mpatie vipeperushi cha injili.
- Mazungumzo yanapogelekea kuelezea matatizo ya ulimwengu au jamii, (Familia mmomonyoko uhalifu madawan.k) uliza: Unafikiri suluhisho la matatizo haya liko wapi? Unajua Biblia inatupa majibu?
- Umewahi kuwa na uhakika kwamba ukifautaenda mbinguni? Unapenda kujua jinsi gain unaweza kuwa na uhakika?
- Unapata wapi pumziko la kiroho?
- Je umewahi kuambiwa namtu yeyote jinsi ya kumjua Mungu? Ungependa kujua biblia inasema nini juu ya hili?



## Hatua ya 14

# Wakati Unaokuja

Jibu Ndiyo (N) au Siyo (S)
____ Unyakuo ni sawa na dhiki.
____ Wakati wa kutisha wa hukumu ya Mungu unawasubiri wasioamini.
____ Wakati wowote Kristo anaweza kuja kutupeleka sisi waumini wake kule aliko.

Wakati mwingine tunapoona mchanganyiko wa dunia, tunajiuliza, hivi ni mambo gani yatakayokuja? Hivi Mungu bado yuko katika kumiliki hapa duniani? Biblia imeweka wazi mpango wa enzi ya Mungu kwa ajili ya mabao yatakayokuja. Somo hili litalengwa juu ya vipengere vya mpango.

## Kalenda ya kinabii

**Unyakuo** | **Ujio wa pili** | Ufufuo wa Wasioamini kwa ajili Ya hukumu ya mwisho **Enzi nyeupe kubwa**

| **Kanisa** | **Dhiki** | **Ufalme wa Millenia** | **Milele** |
|---|---|---|---|
| Wakati Wa sasa | Miaka 7 | Miaka 1000 | **Mbingu** kwa wenye haki |
| | | | **Jehanamu** kwa waliobaki |

Unyakuo: Ufufuo wa Waliokufa katika Krsito; Wakristo watakapokutwa hai watanyakuliwa

Ujio wa pili: Kurudi kwa Kristo duniani; Ufufuo wa waumini kutoka Agano la kale na ateso

### UNYAKUO

Biblia inafundisha kuwa katika kipindi kisichotarajiwa Wakati Ujao, Kristo atakuja kuchukua kanisa lake mbele Uwepo wake. Hii inaitwa Unyakuo. Wakati wowote Kristo Anaweza kuja katika Mawingu kunayakua kanisa. Unyakuo Siyo sawa na Ujio wake wa pili ambao tutajifunza katika Somo linalofuata. 1 Wathesalonike 4:13-18; 1 Wakorintho 15:51-53

Soma 1 Wathesalonike 4:13-18. hapa Paulo anajibu swali, nini hutokea kwa waumini waliokwisha kufa? Hebu tuone namna anavyojibu swali:

1 Nini hutokea tarumbeta ipigwapo na Bwana anapotoka Mbinguni
Mst. 16b ____________________
Mst. 17 ____________________

2 Nani atakuja kutuchukua? Mst.16 ____________________

3. Tutakutana wapi na Bwana huko juu? Mst. 17 ____________________

4 Tutakuwa wapi baada ya Unyakuo? Mst. 17 ____________________
____________________

**FIKIRI JUU YA HILI**

Una watu wowote unaowapenda ambao wamekwisha kufa? Ikiwa walikuwa waumini, unajisikiaje unapotafakari juu ya 1 Wathesalonike 4:13-16?

____________________
____________________
____________________
____________________
____________________
____________________

Je Biblia inafundisha kuwa watu wote wa dini watanyakuliwa?

❏ Ndiyo ❏ Hapana

Je, ni kweli kuwa kuna watu wanaodai kuwa ni Wakrsito na wakati huo huo siyo?

❏ Ndiyo ❏ Hapana

Kunaweza kuwa na watu ndani ya kanisa lako wanaodai kuwa Wakristo, lakini ambao hakika siyo?

❏ Ndiyo ❏ Hapana

Nini kitawatokea unyakuo utakapokuja

____________________
____________________
____________________
____________________
____________________
____________________

**KUENDELEA KUWA IMARA**



**Soma**
**2 Timotheo 1-4**
**na Zaburi 19-21**
**wiki hii (Sura**
**moja kwa siku)**

***Kariri 1 Wathessalonike 4:17***

***Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.***

**KITU CHA KUTAFAKARI**

Wengine wamesikia injili, lakini awamekataa kumpokea Kristo. Wanasema "Kama haya yote kuhusu Unyakuo kweli ni hakiaka na wakati fualani Wakrist wote watapotea, nitampokea Kristo."

Kwa sura ya Biblia inavyosema kuhusu mateso, utasemaje kuhusu watu hawa? Kabla ya kujibu swali soma Ufunuo 20:4 kuona nini kitatokea kwa wengi wanaompkea Kristo wakati wa mateso

__________________________

__________________________

__________________________

__________________________

__________________________

__________________________




Soma 1 Wakorintho 15:51-53 na ujibu maswali yafuatayo:

5. "__________________ wote lakini sote ___________________" Mst. 51
   Neno "Kulala" linarejea kifo. Siyo waumini wote watakufa kwa. Sababu baadhi yao watanyakuliwa kabla ya kifo. Je, Wakristo wote watakaokuwa hai watanyakuliwa

6. Na Unyakuo, wale wapotevu watageuzwa kuwa ___________________

   Na waliokufa watageuzwa kuwa __________________________ Mst. 53

   Unafikiri hii inamaanisha nini? __________________________________

   __________________________________________________________

7. Itachukua muda gani kwa Unyakuo kutokea? Mst. 52 ______________

   __________________________________________________________

   Kwa Ufupi: Wakati wowote Kristo anaweza kuja kunyakua kanisa lake. Kwa kitambo, Waumini waliokufa watafufuliwa, na hatimaye kwa Waumini watakao kuwa bado duniani watabadilishwa, wakipokea miili mipya ambayo hautakuwa na udhaifu tene, maradhi au dhambi.

**DHIKI**

Biblia pia inafundisha pia kuwa baada ya Unyakuo, kutakuwa na miaka saba ya mateso ya kutisha juu ya uso wa dunia yote.

8. Mathayo 24:21 inasema kutakuwa ______________, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Mst. Wa 22 unaonesha kuwa itakuwa mbaya sana kiasi kwmaba hakuna mtu atakayeweza kuishi ndani yake kama isingekuwa kweli kwamba Mungu atasimamisha uharibifu ili kwamba asiharibu maisha yote juu ya dunia.

   **Kitabu cha Ufunuo kinaelezea dhiki kama ifuatavyo**

   - Itaanza baada ya Unyakuo wa kanisa
   - Mungu atatupa ghadhabu yake juu ya uovu wa mwanadamu. (Ufunuo 14:191-20)
   - Kutakuwa na mfululizo wa hukumu (Ufunuo 6, 8-9, 15-16) ambao utajumuisha vita, njaa, mapigo na matetemeko ya ardhi. Zaidi ya nusu ya wakazi wa Ulimwengu watakufa. Theruthi moja ya kijani cha dunia, maji ya kunywa na viumbe wa baharini wataangamizwa. Watu watateswa kwa miezi mitano kwa maumivu makali kiasi kwamba watatmani kufa.
   - Dunia nzima itaangukia chini ya miliki ya Mpinga Kristo, adui aliyetangazwa wa Mungu na Watu wake. (Ufunuo 13:3, 4, 7).
   - Wale watakaochagua kubaki waaminifu kwa Mungu watateswa, wengi mpaka mauti (Ufunuo 6:9-11; 7:9-14; 20:4). Kutakuwa pia na mateso makali kwa Isaraeli. (Ufunuo 12; Mathayo 24).
   - Kutakuwa na Manabii wengi wa Uongo na dini za Uongo, zikihitimishwa na ibada ya Mpiga Kristo. (2 Wathesalonike 2:3-4, 9; Ufunuo 13:8, 11-18).
   - Dhiki itaisha kwa Ujio wa Kristo duniani kuuhukumu uovu na kuanzisha ufalme wake duniani.



## Hatua ya 15
# Mambo zaidi kuhusu wakati ujao

Jibu Ndiyo (N) au Siyo (S)
____ Ujio wa pili utasababisha furaha kuu miongoni mwa wakazi wengi wa dunia.
____ Siku moja Kristo atakuja kuhukumu na kutawala dunia nzima.
____ Wasioamini watahukumiwa na kutupwa katika ziwa la moto.

**UJIO WA PILI WA KRISTO**

Kinyume na Unyakuo, wakati Kristo atakapokuja bila kuonekana na wale wa Ulimwengu, Biblia inazungumuza ujio wa kristo wa kuonekana hapa duniani. Mwisho wa dhiki, wakati dunia itakapokuwa katika kipindi cha kujiharibu yenyewe, Kristo atakuja kuihukumu dunia na kuanzisha miaka yake elfu.

1. Akina nani watauona Ujio wa pili wa Kristo juu ya dunia? Ufunuo 1:7 ______________________________
2. Watu wataupokeaje Ujio wake? ____________________________________

Soma Ufunuo 19:11-16 na ujibu Maswali yafuatayo:

3. Atakuja kwa haki ___________________ na ___________________ Mst. 11
4. Kristo atakanyaga shinikizo la mvinyo ya ____________________ Mst. 15
5. Nanai atakanyaga ujio wake wa Pili? ______________________________
   Kinyume chake, wenye haki, Ujio wake wa pili ni Muda wa kufurahia ambao unaashiria mwisho wa Utawala wa Mpinga Krsito na mwanzo wa utawala wa haki.
6. Mst. wa 11 unamwita ____________________________________________ I
   Ngawa anakuja kuhukumu, hukumu yake siku zote Zinafuatana na ukweli na haki. Kila mmoja atapokea Kile anachostahili.
7. Mst. wa 16 anamwita ____________________________________________
   Kristo ataanzisha ufalme ulio mkamilifu juu ya dunia; Lakini kwanza atauondoa Ullimwengu wa uovu ili kwamba utawala wake kwa watu wote uwe wa amani na haki

Kwa ufupi: Mwisho wa mateso, Kristo atakuja Ulimwenguni Kukamilisha vitu viwili: Kuhukumu na kutawala. Hukumu yake itakuwa ya kutisha juu ya uovu, wakati utawala wake utakuwa mkamilifu, wa haki na wa amani.

**UTAWALA WA MILLENIA**

Utawala wa Kristo utaitwa wa millennia kwa sababu utadumu kwa miaka 1000

8. Shetani atakuwa wapi wakati wa ufalme wa millennia? Ufunuo 29:1-2
   ____________________________________________
9. Isaya 11:4 unelezea Millenia kama wakati wa ______________________
   kwa masikini na ____________________________________ kwa waovu.
10. Ni kwa namna gani amani ya millennia imeelezewa Katika Isaya 11:6?
   ____________________________________________

**FIKIRI JUU YA HILI.**

Kwa kupitia sura ya masharti ya uliwemngu leo, itakuwa rahisi kwa waumini kukatishwa tamaa, wakihofu kuwa Mungu hakika bado yuko katika mamlaka.

Mbali na namna gani vitu vinaonekana, unabii wa kibiblia unatupa mtizamo mpya, unaturuhusu kuona vitu kama vilivyo.

*"… Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande viapnde na kuziharibu, naoa utasimama milele na milele."*
*Daniel 2:44*

*"Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele."*
*Daniel 7:18*



**ANGALIA**

1 Wakorintho 3:11-13 inazungumzia vitu mbali mbali tunavyotumia kujenga maisha yetu. Vitu gani vinatawala katika maisha yako?

❏ Dhahabu, fedha na mawe ya thamani

❏ Mbao, nyasi au majani makavu

NI LAZIMA WOTE TUTATOA HESABU KWA MUNGU



**KITU CHA KUFANYA**

Andika majina ya jamaa zako ambao majina yao hayajaandikwa katika kitabu cha uzima.

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

Unaweza kufanya kitu cha kukusaidia kubadilisha lengo la milele la watu hawa. Mwombe Mungu kwa ajili ya nafasi za kuzungumuza na juu ya Kristo

**KUWA IMARA**

**Soma**
**Ufunuo 19-22**
**Na Zaburi 22-24**
**Wiki hii**
**(Sura moja).**



***Kariri 2 Wakor 5:10***

***Kwa Maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.***

11. Uovu hautaruhusiwa kudhuru au kuharibu kwasababu dunia itajawa na ______________________ Isaya 11:9

**HUKUMU YA KAZI YA KILA MUUMINI**

12. Soma 2 Wakorintho 5:5-10. Paulo siku zote alijaribu kumpendeza Mungu Kwa nini Mst. ______________________

13. Tutapokea ijara gani kwa ajili ya kiti cha hukumu cha Kristo? Mst 10

______________________

14. 1 Wakorintho 3:11-15, Linganisha kazi ya baadhi ya waumini kwenye dhahabu, fedha na mawe ya thamani ambayo yatahimili moto wa hukumu ya Mungu.

Ikiwa kila muumini alichokijenga kitakaa, atapokea ______________

Mst. 14. Ikiwa kazi ya mtu mwingine ikiteketea, atapata ___________

atakuwa ______________________ lakini ni kama tu anayekimbia kama moto. Mst 15. Hii inamaanisha kuwa baadhi ya wale waliookolewa watafika mbele za Mungu na mikono mitupu, bila chochote cha kuweka mbele za Bwana kwa thawabu.

**HUKUMU YA WASIOAMINI MBELE YA KITI CHA ENZI CHEUPE CHA MUNGU.**

Ufunuo 20:11-15 inaelezea hukumu ya kazi ya wasioamini watakaposimama mbele za Bwana.

15. Nani atahukumiwa? Je, yeyote atakwepa hukumu ya mwisho? Mst. 11-13 ______________________

16 Nini kitatokea kwa wale ambao majina yao hayakuandikwa ndani ya kitabu cha uzima? Mst. 15 ______________________

17. Ni kwa namna gani ziwa la moto limelezewa katika kitabu cha uzima? Mst. 15 ______________________

18. Nani mwingine atakuwa katika ziwa la moto? Ufunuo 20:10 ________

**UMILELE**

19. Warumi 8:21 Siku moja viumbe vitaokolewa kutoka ____________ na kuingia katika______________ Baada ya Ufalme wa Millenia na hukumu ya kiti kikubwa cha enzi cheupe, Mungu ataiharibu dunia na kuumba mbingu mpya, dunia mpya na mji mpya, Yerusalemumpya. (Ufunuo 21:1-3). Katika mji huu wa mbinguni, Mungu atakaa na wale ambao wameokolewa.

20. Kutokana na mistari ifuatayo katika ufunuo andika baadhi ya masharti yatakayojitokeza katika Yerusalemu mpya na dunia mpya.

21:4 ______________________

21:27 ______________________

22:3 ______________________

22:5 ______________________

## Kiambatisho cha 1

# Kuyajua Mapenzi ya Mungu

1. Unaamini inawezekana kujua mapenzi ya Mungu? Angalia Zaburi 32:8

2. Uko Tayari kutii mapenzi ya Mungu bila kujali chochote, au unataka kujua mapenzi yake ni nini ili uweze kuamua kama ni njia unayotaka kuiendea? Yohana 7:17

3. Je umewahi kufanya maamuzi ya kukabidhi maisha yako kwa Kristo kikamilifu? Kama siyo, fikiri juu ya Warumi 12: 1-2 na utafute ushauri toka kwa waumini waliokomaa.

4. Je. Kuna dhambi isiyotubiwa bado katika maisha yako? Je unajifnaya kuishi maisha ya kawaida wakati ukimficha Mungu vitu fulani? Kama ni hivyo, chukua muda sasa na utubu dhambi hiyo. Kama hauko tayari kukabiliana dhambi yako, kutafuta kwako mapenzi ya Mungu ni bure. 1 Yohana 1:9; Mithali 28:13; Zaburi 66:18.

5. Je, unatii kile Mungu anachokuamuru kufanya siku kwa siku? Kama sivyo anza leo. Kitu mhimu ni kutii kile ambacho tunajua tayari kuwa ni mapenzi yake, kwa mfano kila amri tunayoiona katika Biblia ni kiashiria cha wazi cha kile anachokitaka tukifanye.

6. Je, tayari umeifanya akili yako na haiwezi kupendezwa na kupokea ushauri? Je unajali Biblia inavyosema juu ya maamuzi unayotegemea kuyafanya? Omba, ukimwomba Mungu kukupa moyo wa kupenda kufanya mapenzi yake bila kujali ni ya aina gani. Wafilipi 2:13

7. Je, unaomba hasa hasa juu ya maamuzi yako utakayoyafanya hivi karibuni? Andika mawazo yako juu ya maamuzi yako uanayotaka kuyafanya, na uuanze kuomba kwa ajili ya hayo. Omba kwa imani, ukiamini kuwa Mungu atakupa mwongozo. Yakobo 1:5-7, Mariko 10:51.

8. Vipi kuhusu maisha yako ya ucha Mungu? Je, uko katika ushirika na Kristo kila wakati siku nzima? Unasoma Biblia kila siku na kuomba? Kama sivyo, amua kuanza leo, kadiri unavyojaza kichwa chako na neno la Mungu, utajifunza kufukiri na kufanya maamuzi kibiblia.

9. Je Mungu amzungumuza na wewe kwa nia ya kujifunza kutoka neno lake? Je unajisikia kuwa baadhi ya mistari inayokuita kufanya mabadiliko katika mfumo wako wa maisha au kufany marekebisho katika njia uliyoichukua? Andika kwenye daftari kile unacho fikiri Mungua nakwambia. Kama unasoma Maandiko na bado usisikie kuongozwa, endelea kusoma na usubiri kwa uvumilivu.

10. Je, una habari zote muhimu ili kukuwezesha kufanya maamuzi? Kama sivyo, tafuta nini unachokihitaji kukijua kuweza kufanya maamuzi ya mwenye taarifa

11. Andika orodha ya nathari na majazo wa lugha katika maamuzi ambayo umekuwa ukifikir. Tathmini kila faida na hasara kupitia maandiko. Vitu haviko siku zote vinavyoonekana katika mwonekano wake wa mwanzo.

12. Je, akili yetu ya kawaida inakwambia nini?

13. Unataka kufanya nini? Je, una upendeleo maalumu? Zaburi 37:4

14. Kabla ya kufanya maamuzi, jiulize ni kwa namna gani itakuathiri kiroho, kimwili, kihisia, kijamii na kiakili. Tafakari juu ya 1 Wakorintho 6:12. Ukweli kwamba kitu fulani hakijakataliwa moja kwa moja katika maandiko, siyo lazima ioneshe kuwa ni sahihi au batili.

15. Je, umewahi kufikiria juu ya maamzui ambayo ama unayachukua utaleta vitu vingine vya kiafya katika maisha yako. Je, itakupeleka kuelekea maisha ya kupenda vitu au ya kihisia. Je, itakuletea amani kwa wingi au kidogo.? Mariko 4:19

16. Ni kwa namna gani mawazo yako yataathiri wengine? Je, haitasababisha wengine kukwazika? 1 Wakorintho 10:31.

17. Je, umewahi kutafuta ushauri wa waumini waliokomaa? Mithali 15:22

18. Je, maamuzi ambayo unataka kuyafanya yanaharibu amri yoyote ya Mungu?

19. Kama huna hakika juu ya sababu ya namna ya kufanya, je, uko tayari kusubiri kwa imani mpaka Mungu atakapokupa amani na na mambo yanayofaa? Waebrania 10:36

20. Kama una amani ya ndani na ushawishi kuwa ni kwa mapenzi ya Mungu, endlea kwa kujiamini. Tenda kwa imani yako. Warumi 14:23; Waebrania 11:6

## Kiambatisho cha 2

# Ujumbe wetu ni nini?
# Ufupisho wa Injili

Kuna njia nyingi za kufikisha injili. Tunaweza kutumia mojawapo lakini upo ujumbe wa msingi wa msingi ambao wote wanapaswa kuelewa ili waokolewe. Mpango ufuatao wa wokovu umechukuliwa kutoka Kanuni Nne za Kiroho (The four Spiritual Law).

1. Mungu anawapenda na ana mpango kwa maisha yangu

   Yohana 3:16 Mungu anatupenda

   Yohana 10:10b Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yetu

   Kwa nini watu wachache wamepitia uzoefu wa upendo wa Mungu na mpango kwa ajili ya maisha.

2. Sisi ni wenye dhambi na tumetengwa toka kwa Mungu

   Warumi 3:23 Wote tumetenda dhambi

   Warumi 6:23 Madhara ya dhambi ni kifo cha kiroho na kutengwa milele toka kwa Mungu

   Waefeso 2:8-9 Wokovu ni kwa imani pekee. Hatuwezi kujiokoa wenyewe kupitia matendo mema.

3. Kristo ni toleo pekee la Mungu kutuokoa, Alikufa katika nafasi yetu.

   Warumi 5:8 Kristo alikufa kwa ajili yetu

   2 Wakorintho 5:21 Alichukua dhambi zetu ili kwamba tutangazwe kuwa wenye haki

   Yohana14:4 Yesu ni njia pekee ya wokovu

   1 Wokorintho 15:3-6 Kristo alifufuliwa kutoka wafu

4. Tunapaswa kumpokea Kristo kama mwokozi wetu

   Yohana 1:12 Tunapaswa kumpokea Kristo ili tuwe watoto wa Mungu

   Ufunuo 3:20 Tunapaswa kumkaribisha Kristo kuja katika maisha yetu

# Kiambatisho cha 3

Kata katika mistari.  Tembea na kadi hizi na ukariri mistari hiyo ya Biblia

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Wakolosai 3:1 Hatua Ya 4*<br><br>*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu.* | *Mathayo 5:23-24 Hatua Ya 8*<br><br>*Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yak, kisha urudi uitoe sadaka yako.* | *2 Timotheo 2:15 Hatua Ya 12*<br><br>*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubalika mbele za Mungu, mtenda kazi asiye tahayari, akitumia halali neon la kweli.* | *2 Wakor 5:10 Hatua Ya 15*<br><br>*Kwa Maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.* |
| *Mathayo 20:27-28 Hatua Ya 3*<br><br>*…….na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu;kama vile mwana waAdamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.* | *Wakolosai 3:13 Hatua Ya 7*<br><br>*Mkichukuliana na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasame-he ninyi vivyo hivyo ninyi.* | *1 Wakoritho 10:23 Hatua Ya 11*<br><br>*Vitu vyote ni halali bali si vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali bali si vyote vijegavyo.* | *1 Wathessalonike 4:17 Hatua Ya 14*<br><br>*Kisha sisi tulio hai, tuliosalia,tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.* |
| *Mathew 11:29 Hatua Ya 2*<br><br>*Jitieni Nira yangu, na mjifunze kutoka kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo;nanyi mtapata raha nafsini mwenu;* | *Waefeso 6:11 Hatua Ya 6*<br><br>*Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuzipinga hilka zote za Shetani.* | *2 Wakoritho 9:6 Hatua Ya 10*<br><br>*Kumbuka hili: Apandayre haba atavuna haba, na apanaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.* | *Warumi 10:15 Hatua Ya 13*<br><br>*Watahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa "Jinsi gani ilivyo mizuri miguu yao wapelekao habari njema"* |
| *Yohana 5:39 Hatua Ya 1*<br><br>*Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake;na hayo ndiyo yanayonishuhudia.* | *Yakobo 4:7 Hatua Ya 5*<br><br>*Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia.* | *1 Petro 1:14-15 Hatua Ya 9*<br><br>*Kama watoto wakutii msijifananishe Na tamaa zenu za kwanza, Bali Kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, hivyo iweni watakatifukatika mwenendo wenu.* | |

# Cheti

Cheti hiki kimetunukiwa kwa

________________________________________

ambaye amekamilisha kwa kufaulu masomo yote katika kitabu hiki

## Maisha Mapya Ndani Ya Kristo Toleo la 2

### Hatua zaidi za kimsingi katika maisha ya Kikristo

Jitieni Nira yangu, na mjifunze kutoka kwangu; kwa
kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo;
nanyi mtapata raha nafsini mwenu;" Mathew 11:29

______________________________

Mwalimu

____________________

Tarehe